# Nipashe

Ijumaa Agosti 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581035

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT

1,021,208,577/-

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Chongolo** ataka sekondari za mradi wa maboresho ziwe na mchepuo wa kilimo

UKURASA 3



UKURASA 21

**ANCELOTTI AKICHAMBUA KIWANGO CHA BENZEMA**

# HADHARI YA NJAA

• **Rais** Samia ataja hatua za serikali akitaka wananchi...*uk. 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na wananchi baada ya kutoka kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa Barabara ya Sawala-Mkonge-Iyegea, yenye urefu wa Km 40.7 kwa kiwango cha lami mkoani Iringa jana. **PICHA: IKULU**



## NHIF yakiri kuelemewa gharama za matibabu

UKURASA 2

UKURASA WA 4



### AJALI YAUA WATU SITA

WATU sita wamefariki dunia baada ya gari dogo aina ya Toyota RAU walilokuwa wamepanda kwa safari ya kutoka Arusha kwenda Wilaya ya...

UKURASA WA 9

### ALIYEJITOA UCHAGUZI WA CCM ASHINDA

KATIKA hali iliyowashangaza wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi ya Kata ya Kilago, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama...

## Taharuki utangazaji matokeo uchaguzi mkuu nchini Kenya



UKURASA 3


MICHEZO SIMBA, YANGA HESABU KALI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Rais Samia ataja mikakati serikali kukabili baa la njaa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Tanzania imeanza mikakati ya kukabiliana na baa la njaa linalohofiwa kuikumba dunia kutokana na athari za UVIKO-19.

Pamoja na mikakati hiyo, amewataka wakazi wa mkoa wa Njombe kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara wakati serikali ikiendelea kuboresha mazingira ya upatikanaji wa pembejeo kwa bei nafuu na masoko.

Rais aliyasema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati wa ziara yake ya kikazi katika mikoa ya Iringa na Njombe maeneo ya Nyololo na Sawala wilayani Mufindi na Makambako mkoani Njombe.

"Baada ya Uviko-19 kutakuwa na tatizo la njaa duniani. Hata hivyo, Tanzania Mungu ametubarikia ardhi nzuri na hali ya hewa nzuri. Tuzalishe chakula cha kututosha sisi wenyewe ili tujihakikishie usalama wa chakula na majirani zetu nchi zenye uhitaji," alisema.

Samia alisema serikali imeendelea kujizatiti kwenye kilimo ili kuwa na uhakika wa chakula.

"Tunaendelea kuongeza viwanda ili wakulima muongeze mazao yenu thamani kulingana na mwenendo wa soko la kimataifa. Kwa Iringa tutawaachia kiwanda hiki cha parachichi hapa Mufindi," alisema.

Rais alisema licha ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kusifika kwa kilimo cha parachichi, bado wakulima hawanufaiki kutokana na mazao yao kukosa ubora kwa kuwa hayaongezwi thamani.

Katika hatua nyingine, aliwaagiza madiwani kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato katika maeneo yao ili kuleta maendeleo kwa wananchi.

Alisema ni lazima madiwani wasimamie mapato ya ndani kikamilifu na kudhibiti upotevu ili kuwasaidia wananchi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

**KAZI IENDELEE**

Akiwa Makambako, alisema anaposema kazi iendelee, anamaanisha kuongeza kasi ya uzalishaji, hivyo anayelima alime kwa kuwa kuna mazingira mazuri na mbolea na pembejeo zitapatikana.

"Tumefungua soko kisha lima weka chakula cha kutosha nyumbani, uza kinachobaki urudishe pesa yako uingie tena shambani. Niwaombe wana Njombe nendeni kachapeni kazi tuzalishe kwa maendeleo ya taifa letu," alisema.

**RAIS HAJAFIKA**

Mbunge wa Mufindi Kusini, David Kihenzele, alimweleza rais kuwa kwa zaidi ya miaka 50 hakuna Rais aliyetembelea Kijiji cha Sawala hali inayozorotesha maendeleo.

Akizungumza muda mfupi baada ya Rais kuweka jiwe la msingi katika ujenzi wa barabara ya Sawala -Iyegea kiwango cha lami, Kihenzile alisema kulikuwa na kudorora kwa maendeleo kutokana na viongozi wa kitaifa kutofika katika eneo hilo.

"Miaka 50 sasa tangu mwaka 1972 alipotembelea Rais Julius Nyerere hakuna aliyefika Sawala wewe ni wa pili. Hii imekuwa neema sana. Hakika umetatua kilio cha wananchi cha muda mrefu cha ukosefu wa miundombinu ya barabara, "alisema.

Awali, akizindua mradi huo wa ujenzi wa barabara, Rais Samia alisema kwa sasa serikali inawekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara ili kukuza sekta za kilimo na viwanda.

■**Imeandikwa na Elizabeth John (Njombe), Martha Sambo na Godwin Fransis (Iringa).**




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Taaluma), Prof. Bonaventure Rutinwa na Mtunzi wa kitabu kipya cha watoto cha The African Alphabet, Kemilembe Mugangala, wakiwafundisha watoto wadogo kusoma kwa kutumia kitabu hicho, baada ya kukizindua, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NHIF yakiri kuelemewa gharama za matibabu

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umesema magonjwa yasiyo ya kuambukiza, yamekuwa mzigo mkubwa kwao kutokana na kutumia gharama kubwa kulipa kwa watoa huduma ya afya wanaowahudumia wateja wao.

Umebainisha kwa mwaka wa fedha 2021/22, ulitumia Sh. bilioni 99 sawa na asilimia 18 ya malipo yao yote kwa watoa huduma za afya kuhudumia wanachama wao.

Mkoani Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alipozungumza na waandishi kuhusu kazi zinazofanywa na mfuko huo, alisema kwa kuzingatia mwenendo huo, kuna haja serikali kuangalia afua zingine za kitaifa za kupambana na magonjwa hayo.

"Katika kipindi kilichopita, 2021/22 tunaona bado fedha nyingi inatumika kwenye magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza. Kwa hiyo, mwelekeo wa serikali ni sahihi katika kuongeza jitihada kupambana na magonjwa hayo.

"Mathalani, kwa mwaka uliopita fedha nyingi tumelipia kwenye dawa za saratani, na tunafahamu ni magonjwa ambayo yanatokana na aina ya maisha tunayoishi na vyakula tunavyokula. Pia, fedha nyingi tumelipa kwenye gharama za kuchuja damu, pale ambapo inaonekana figo haiwezi kufanya kazi kama inavyotarajiwa, huwa kuna hiyo huduma," alifafanua.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, matibabu ya kusafisha damu yaliigharimu NHIF Sh. bilioni 35.4 zilizolipwa kwa watoa huduma waliohudumia wanachama wa mfuko huo.

"Kwa hiyo, kwa kifupi utaona namna gani magonjwa hayo yameanza kuwa mzigo mkubwa, ni suala la kitaifa linazungumzwa, lakini na sisi kama mfuko kwa wanachama wetu tunaliona bayana kwamba sasa wanachama wetu wengi tunagharimia pesa nyingi kuelekea huko.

"Kwa hiyo, ni jukumu letu sisi kama mfuko kuunga mkono jitihada za serikali katika kupambana na magonjwa haya kwa sababu ikiendelea hivi, ni wazi mzigo ni mkubwa kwa mfuko. Mtakumbuka zamani tulikuwa tunaugua malaria siku tatu, ya nne umeenda kazini na umemalizana na dozi, lakini leo hii ukianza 'dyalisis' (usafishaji wa damu) ina maana ni 'life time' (maisha yote)."

"Na gharama za 'dyalsis' inakwenda kati ya Sh. 240,000 au Sh. 250,000 kwa 'session' (kipindi) moja na unaweza kuambiwa 'sessions' nne kwa wiki. Kwa hiyo, ina maana ni Sh. milioni moja kwa wiki na ikienda kwa mwaka ni Sh. milioni 52.

"Katika hali ya kawaida ni gharama kubwa sana. Kwa hiyo, tunaunga mkono na tunaipongeza serikali kwa kutumia macho kwenye eneo hili la kupambana na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza, kwa sababu ni mzigo mkubwa," alisema.

Pia, alisema mpaka sasa mfuko huo unatumia fedha nyingi katika matibabu ya watoto na wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60.

Konga alisema kwa mwaka wa fedha uliopita, hospitali zilizolipwa fedha nyingi kutokana na kutoa huduma kwa wanachama wake ni za kanda kwa asilimia 23 zikifuatwa na hospitali za rufani za mikoa kwa asilimia 20.

"Hii ni tofauti na zamani ambapo kiwango kikubwa cha fedha kilikuwa kikilipwa katika hospitali za taifa (Muhimbili na Mirembe), kwa maana sasa wananchi wanapata huduma karibu na maeneo yao na siyo lazima wasafiri tena umbali mrefu.

"Mathalani huduma za saratani, siyo lazima mtu aende (Taasisi ya Saratani) Ocean Road kupata huduma hizo, na hayo yote yanaonekana kwa sababu serikali imewekeza katika eneo hilo," alisema.

Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi kujiunga na NHIF ili iwe rahisi kuwahudumia, akibainisha kwa sasa wanachama wa mfuko ni asilimia nane (milioni 4.8 hadi Juni mwaka huu ya Watanzania wanaopata huduma kwenye vituo 9,188, huku asilimia sita ya Watanzania wakiwa katika Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na asilimia moja sekta binafsi.

"Ndiyo maana unakuta katika baadhi ya nchi, wanachama wanakiwa ni wengi hata kufikia asilimia 90, inapofikia katika hatua hii inakiwa rahisi kuwahudumia lakini wakijiunga wachache ni changamoto," alisema.

Pia alisema wanatarajia kutoa mwongozo wa bei na utaratibu wa usimamizi wa huduma za bima ya afya nchini ili kudhibiti upangaji holela wa bei za dawa.

Vilevile, alisema wamebaini kuwapo udanganyifu mkubwa ikiwamo watu kuwa na vyeti feki vya ndoa, baadhi ya vituo kudanganya na kila wanapobaini wanachukua hatua kali ikiwamo kuwafikisha mahakamani.

# Chongolo ashauri shule 124 kuwekwa mchepuo kilimo

**Na Mary Geofrey,** MUHEZA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameshauri shule zote 214 zinazojengwa nchini kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP), kuwa na mchepuo wa Kilimo.

Alisema kuwapo kwa masomo hayo, kutasaidia vijana wanaohitimu elimu ya sekondari kuwa na ujuzi wa kilimo utakaowasaidia kujiajiri na kukuza sekta hiyo nchini.

Chongolo alitoa pendekezo hilo jana wilayani Muheza mkoani Tanga, wakati akikagua mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Kisiwani, akiwa kwenye ziara yake ya kukagua ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo na kuhamasisha watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Alisema atazungumza na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda ili kuingiza somo hilo la kilimo litolewe katika shule hizo zinazojengwa nchini.

"Ni muhimu madarasa haya yaliyojengwa kwa fedha za serikali Sh. milioni 600 kwa kila moja, kutumika kufundisha vijana wetu masomo ya kilimo hasa kwa kuzingatia kuna chumba cha maabara ya masomo ya kilimo yanahitaji kuwa na maabara na shule hizi zimekidhi vigezo vyote," alisisitiza.

Alisema serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imetoa Sh. bilioni 100.58 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari mpya 214 ambazo zinajengwa kwenye kata za majimbo yote nchini.

Chongolo alimuagiza Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba na Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Halima Bulembo, kufuatilia kwa Wakala wa Misitu (TFS), kuomba kuongezewa eneo kwa ajili ya kujenga majengo mengine ya kidato cha tano na sita, bwalo la chakula na nyumba za walimu.

Alitoa agizo hilo baada ya mbunge wa jimbo hilo, Khamis Mwijuma, kumweleza kuwa eneo hilo la ekari tatu lililotolewa na mkazi wa eneo hilo kwa ajili ya kujenga shule hiyo kumalizika na eneo jirani ni la msitu wa Amani.

Chongolo alishauri shule hiyo ikimalizika ipewe jina Manofu ambalo ni la mkazi aliyetoa eneo hilo kwa lengo la kuthamini mchango wake kwa jamii na kuhimiza jamii hiyo kujitolea kwenye miradi ya maendeleo.

Awali, Mwijuma alisema shule hiyo itapunguza adha ya wanafunzi kutembea kilometa 23, kufuata masomo kata za jirani na kuiomba serikali kuiongeza Sh. milioni 130 kwa ajili ya kumaliza ujenzi uliobaki.

Awali, Diwani wa Kata hiyo, Shaban Mussa, alisema licha ya serikali kutoa Sh. milioni 470 kati ya milioni 600 zinazohitajika, wananchi hao wamechangia ujenzi huo Sh. milioni 26.

Alisema walianza kujenga madarasa mawili yenye thamani ya Sh. milioni 15 na kutoa nguvu kazi zao katika kazi ya ujenzi inayoendelea.

Naye Mkuu wa mkoa huo, Omary Mgumba, aliahidi kukaa na uongozi wa wilaya na kamati ya ujenzi kufahamu sababu za ujenzi huo kuwa nyuma kulinganisha na maeneo mangine nchini ambako walipokea fedha za ujenzi mwezi Januari, mwaka huu.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, akitumia mti kujizuia kuteleza kwenye matope, huku akiongozana na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamis Mwinjuma (mwenye shati la njano), pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba (kulia), baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Kisiwani, Kata ya Kisiwani, Wilaya ya Muheza jana. **PICHA: ADAM MZEE**

# Taharuki utangazaji matokeo uchaguzi Kenya

**Na Maulid Mmbaga**

TAHARUKI imeibuka kutokana na kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi mkuu wa Kenya uliofanyika Jumanne wiki hii, huku kila chombo cha habari kikitoa matokeo yake.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka ya Kenya (IEBC), Wafula Chebukati, amewataka wananchi kutokuwa na hofu kutokana na tofauti hizo, huku akisisitiza kuwa matokea ya mwisho yatatangazwa na tume hiyo.

Kwa mujibu wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Chebukati alisema alikuwa na matumaini kwamba vyombo vya habari vingeungana na kuanzisha kituo kimoja cha kujumlisha matokeo ya kura lakini haikuwa hivyo.

"Nataka tu kuwafahamisha Wakenya kwamba tangazo la mwisho la matokeo ya urais litafanywa na msimamizi wa uchaguzi hapa Bomas. Tunatumai kufikia mwisho wa kujumlisha, yatakuwa yanafanana.

"Kusiwe na hofu kuhusu tofauti tunazoziona kwenye vyombo vya habari kwa sababu mbinu zao zinatofautiana. Mwisho wa siku matokeo yataainishwa kwa sababu yanatoka chanzo kimoja," alisema.

**MCK YAINGILIA**

Baraza la Habari la Kenya (MCK) lilielezea wasiwasi kuhusu utofauti katika utangazaji wa matokeo ya uchaguzi mkuu unaofanywa na vyombo vya habari nchini humo.

Lilisema ucheleweshwaji wa matokeo rasmi kutoka kwa IEBC ulisababisha kuenezwa kwa taarifa nyingi potofu na baraza hilo sasa linashughulikia tatizo hilo.

MCK ilisema inafanya majadiliano na muungano wa wamiliki wa vyombo vya habari pamoja na wahariri ili kubuni njia ya pamoja ya kutangaza matokeo kati ya vyombo hivyo vya habari.

Ofisa Mtedaji Mkuu wa MCK, David Omwoyo, alisema hatua hiyo inachangia kuibua taharuki kati ya umma wakati huu ambapo subira ya muda mrefu ya matokeo ya uchaguzi inawatatiza wengi.

**UN YAPONGEZA**

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, jana aliwapongeza Wakenya kwa kuhakikisha uwepo wa amani wakati wa uchaguzi.

Guterres aliipongeza IEBC na serikali ya Kenya kwa kuhakikisha wapigakura wanapata fursa ya kutekeleza haki yao ya kikatiba kwa uhuru.

Pia aliwataka wanasiasa na wapigakura kuwa watulivu na kujizuia wakati wakisubiri mchakato wa uchaguzi kukamilika.

Asilimia 65.4 ya wapigakura waliojiandikisha, ambao ni milioni 22 nchini humo, ndio walijitokeza kupiga kura, tofauti na mwaka 2017 ambapo asilimia 80 ya waliojiandikisha walipiga kura.

**MTUHUMIWA ASHINDA**

Mbunge wa Kimilili, Didmus Barasa, wa chama cha United Democratic Alliance, ambaye ametoroka kwa tuhuma za kumuua kwa kumpiga risasi msaidizi wa mpinzani wake, Brian Khaemba, wa chama cha DAP-K Jumanne jioni, alitangazwa kushinda kwa kupata kura 26,000 dhidi ya kura 9,000 za Khaemba.

Baadhi ya wakazi wa eneo hilo akiwamo Wasilwa Wafula, walimtetea mbunge huyo dhidi ya madai hayo, wakisema alikuwa anajilinda.

"Barasa alikuwa anajilinda, hii si mara ya kwanza kwa watu kujaribu kumuua," alisema Wafula.

Mwendesha Mashtaka, Noordin Haji, aliwataka polisi kumkamata mbunge huyo na kurekodi taarifa, huku polisi wakieleza kuwa bado hawajamkamata na simu yake imezimwa.

**WANAOPINGA WAFUATE SHERIA**

Kiongozi wa Waangalizi wa Uchaguzi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais mstaafu wa Tanzania, Jakaya Kikwete, aliwataka wagombea ambao hawatakubaliana na matokeo, waende mahakamani badala ya kutumia njia zisizo sahihi.

Alisema uchaguzi ulifanyika kwa amani, utulivu na uwazi kutokana na maandalizi yaliyofanywa na taifa hilo pamoja na IEBC.

"Tunawasihi mwendeleze amani na utulivu baada ya matokeo kutangazwa. Kama mtu atakuwa na pingamizi kuna mwanya wa kisheria, hivyo wachukue mkondo huo," alisema Kikwete.

Hadi sasa kura hizo zinaonyesha kuwapo kwa ushindani mkali wa wagombea wa urais kati ya Naibu Rais William Ruto na mwanasiasa mkongwe, Raila Odinga.

**■Imeandaliwa kwa msaada wa mitandao mbalimbali ya kimataifa.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA NIA YA UGAVI WA VIFAA VYA ZEGE**

**KUMB : ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0001-00.**

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, ununuzi na Ujenzi wa Jeti na Vifaa vya Kupakia kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni wataalamu wenye uzoefu kueleza nia yao kwa:

**Ugavi wa vifaa vya zege kama vile kokoto, mchanga, saruji, vichanganyishi na vipozeo vya zege**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufuo wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni kutoka eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
Kutafuta makampuni ambayo yanaweza kutoa maelezo yakinifu yakiufundi na vifaa ambavyo vinakutumika katika mchakato wa kutengeneza zege.

**Vifaa ambavyo vinahitajika:**
- Kokoto (kiwango cha juu cha DN 32.5 mm),
- Mchanga (mchanga wa mtoni na/au mchanga uliosagwa na karasha);
- Saruji,
- Vichanganyishi,
- Vipozeo vya Zege (Mabonge ya barafu).

**SIFA BAINIFU:**
Makampuni yenye nia yanaalikwa kuandika ombi lao kwa kuambatanisha:
- Rekodi inayofaa inayoonyesha uzoefu isiopungua miaka mitano (5) katika usambazaji wa nyenzo thabiti za kutengenezea zege,
- Wafanyakazi waliohitimu na kuthibitishwa kufanya kazi za Uthibiti Ubora/ Uthibitishaji Ubora (QA/QC);
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kifedha na rasilimali za kutosha kufanya/ kusimamia kandarasi husika,
- Kuzingatia kanuni za petroli na matumizi yarasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha nia, unashauriwa.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com** **(Ukubwa wa Barua Pepe: MB 20 & viambatanishi lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza)** mnamo au kabla ya **tarehe 26 Agosti 2022, Saa 6 mchana kwa saa za Tanzania**

Makampuni yanayokidhi vigezo yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

216985902



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua katika barabara ya Matosa, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TAKUKURU yanasa mbinu za rushwa ya ngono vyuoni

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga imeweka hadharani baadhi ya mbinu wanazotumia baadhi ya wahadhiri wa vyuo vikuu kuomba rushwa ya ngono kwa wanafunzi wao.

Mbinu zilizobainishwa kutumiwa na wahadhiri hao ni pamoja na kuwafelisha makusudi wanafunzi, hasa wa kike ili walazimike kurudia mitihani husika na katika harakati za kujinasua, wanajikuta wananasa kwenye mitego ya walimu wao.

Taasisi hiyo imesema baadhi ya wahadhiri wanawatisha wanafunzi wao kuwa wasipowakubali kimapenzi, watahakikisha hawafaulu mitihani yao.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Shinyanga, Donasian Kessy, alibainisha hayo jana alipoitoa taarifa ya utekelezaji wa kazi zao katika kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu.

Alisema kwa kipindi hicho wametoa elimu maeneo mbalimbali ya mapambano dhidi ya rushwa, ikiwamo kupinga rushwa ya ngono vyuoni mkoani humo na kubaini mbinu ambazo wamekuwa wakizitumia wahadhiri kuomba rushwa ya ngono kwa wanafunzi.

"TAKUKURU mkoani Shinyanga tulitoa elimu ya rushwa ya ngono vyuoni kupitia kampeni ya 'Vunja Ukimya Kataa Rushwa ya Ngono' katika vyuo vitatu ambavyo ni VETA, Ushirika na Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Buhangija na kutoa elimu kwa vijana 541.

"Mbinu ambazo tulizibaini wanazitumia wahadhiri katika kuomba rushwa ya ngono kwa wanafunzi ni kuwafelisha mitihani yao kwa makusudi, husussani kwa wanafunzi ambaye mhadhiri anamtaka kimapenzi na kumtishia akishindwa tena atafukuzwa chuo na hatimaye kufanya naye mapenzi," alifafanua.

Alisema kuwa kutokana na elimu ambayo wameitoa kwa wanafunzi vyuoni, wanatarajia kupata taarifa nyingi juu ya aina hiyo ya rushwa ili wawakamate wahusika na kuwachukulia hatua.

Katika hatua nyingine, Kessy alisema walifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha katika miradi 17 ya maendeleo kupitia fedha za UVIKO-19 yenye thamani ya Sh. bilioni 13.7 na kubaini minne kati yake ilikuwa na dosari.

Alisema miradi hiyo haiendani na thamani halisi ya fedha na kuagiza ifanyiwe marekebisho.

Aliongeza kuwa walifanya uchambuzi wa mifumo kuhusu ujenzi wa vyumba vya madarasa kupitia fedha za UVIKO-19 na uendeshaji na usimamizi wa jumuiya za watumiaji maji ngazi za jamii katika Halmashauri ya Msalala, Ushetu na Kahama na kubaini kuwapo na mianya ya rushwa.

Alisema kwa kipindi hicho walipokea taarifa 29 za malalamiko zilizohusu rushwa katika serikali za mitaa, ujenzi, polisi, elimu, biashara, afya na taarifa 18 uchunguzi wake unaendelea.

Alisema kati ya taarifa hizo, zipo ambazo uchunguzi wake umekamilika na nyingine tayari zimefikishwa mahakamani, pia walikuwa na kesi 10 mahakamani na kati yake, saba walishinda na watuhumiwa kutiwa hatiani na kulipa faini, huku mtuhumiwa mmoja akishindwa kulipa na hivyo kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka mitatu.

Kessy alitoa wito kwa wananchi mkoani Shinyanga pamoja na wanafunzi kuendelea kutoa taarifa juu ya vitendo vya rushwa ambavyo vimekuwa vikiwanyima kupata haki zao.

Baadhi ya wanafunzi ambao wanasoma Chuo cha St. Joseph Tawi la Shinyanga, walidai kuwapo baadhi ya wahadhiri wanaowaomba rushwa ya ngono.

Mwaka 2019, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu rushwa ya ngono vyuo vikuu ikianika namna inavyofanywa na mhadhiri kwa mwanafunzi; mwanafunzi kwa mwanafunzi; mhadhiri kwa mhadhiri; na mhadhiri/ofisa utawala chuoni dhidi ya mfanyakazi wa chini chuoni.

# Ajali ya gari yaua watu sita Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WATU sita wamefariki dunia baada ya gari dogo aina ya Toyota RAU walilokuwa wamepanda kwa safari ya kutoka Arusha kwenda Wilaya ya Nzega mkoani Tabora, kuacha njia na kugonga gema kisha kupinduka mara tatu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi wa Polisi Stella Mutabihirwa, akizungumza na Nipashe jana mjini hapo, alisema ajali hiyo ilitokea Agosti 9, mwaka huu saa 10:15 jioni katika Kijiji cha Igugumo Shamba, Wilaya ya Mkalama mkoani hapo.

Alisema gari hilo lenye namba za usajili T631 CVN lililokuwa linaendeshwa na Adramu Saimon, lilipoteza mwelekeo na kugonga gema lililoko pembeni mwa barabara na kupinduka kutokana na mwendo kasi wa dereva huyo.

Kamanda Mutabihirwa alisema baada ya ajali hiyo, watu watano walifariki dunia papo hapo huku dereva wake akipoteza maisha wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Singida maarufu Mandewa.

Aliwataja wengine waliofariki dunia katika ajali hiyo kuwa ni: Kelvin Michael (43), mkazi wa Kambarage mkoani Arusha; Shufaa Said Athuman (30), mkazi wa Mwanza; Nyahisi Ngolwa, mkazi wa Bunda; Kashinde Khamis (30) na abiria mwingine ambaye alikuwa hajatambuliwa kwa jina.

Kamanda Mutabihirwa alitoa wito kwa madereva wa vyombo vya moto wanapoendesha, kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizokuwa za lazima.

# Wawekezaji Saudia waona fursa nchini

**Na Romana Mallya**

UJUMBE wa wafanyabiashara kutoka Saudi Arabia uko nchini kusaka fursa za uwekezaji katika sekta za kilimo, ufugaji wa samaki na mifugo.

Ujumbe huo ambao ulipokewa jana jijini Dar es Salaam na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), unatafuta maeneo ili kuanzisha uwekezaji utakaosaidia kuimarisha uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya chakula nchini Saudi Arabia.

Katika kikao cha pamoja na ujumbe huo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Revocatus Rasheli, aliikaribisha timu hiyo iliyojumuisha watu 14 ambao ni wafanyabiashara na maofisa kutoka serikali ya Saudi Arabia.

Rasheli alisema wafanyabiashara hao wameonyesha nia ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo na ufugaji.

"Katika majadiliano yanayoendelea, TIC imeratibu na imeleta taasisi mbalimbali zinazofanya kazi za kilimo na ufugaji kibiashara. Tumewaonyesha maeneo mbalimbali ambayo wanaweza kuanzisha miradi yao ya uwekezaji," alisema Rasheli.

Aliwaambia wawekezaji hao kuwa Tanzania imebarikiwa kuwa na fursa mbalimbali katika maeneo ya uanzishaji wa viwanda vya kusindika nyama na samaki, viwanda vya ngozi, ufugaji, viwanda vya kusindika maziwa pamoja na ardhi kubwa kwa ajili ya kilimo.

"Saudi Arabia na Tanzania tuna fursa nyingi, lakini bado hatujazitumia kikamilifu. Naamini tunaweza kufanya vizuri zaidi kwa sasa na nitoe wito kwa mamlaka za serikali katika nchi zote mbili kushirikiana ili kuruhusu kuwa na mtiririko mzuri wa bidhaa na huduma kati ya pande hizi mbili," alisema.

Pia alisema kwa sasa Tanzania inajenga bandari kubwa ya uvuvi katika wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi ambayo inahitaji uwekezaji katika miundombinu kama vile uanzishaji wa viwanda vya usindikaji na kutengeneza barafu, maghala ya kuhifadhia maji baridi na miradi mingine mingi inayohusiana nayo.

Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia, Ali Mwadini, alisema ziara hiyo ni sehemu ya mwitikio wa jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuvutia wawekezaji kutoka pande zote za dunia pamoja na ziara iliyofanywa nchini humo na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula.

Alisema nchi hiyo ya Mashariki ya Kati ina wakazi milioni 35 lakini bado haijafikia uzalishaji wa kutosha kulingana na mahitaji yake, jambo linalowasukuma wawekezaji kutafuta maeneo zaidi ya uwekezaji ili kuzalisha mazao na kuimarisha usalama wa chakula.

Akizungumza kwa niaba ya ujumbe huo, Makamu wa Rais anayeshughulikia Mauzo na Maendeleo ya Biashara kutoka Shirika la Kilimo na Mifugo la Saudia (SALIC), Mhandisi Faisal Almangour, alisema wako nchini kuangalia fursa na wana nia ya kuwekeza Tanzania.

"Mbali na kuanzisha miradi ya uwekezaji, pia tutawaunganisha wazalishaji wa Tanzania na wanunuzi na fursa za masoko nchini Saudi Arabia," alisema.

# Mabula aonya viongozi vijiji, vitongoji kugawa ardhi holela

**Na Munir Shemweta,** BAGAMOYO

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewaonya viongozi wa vijiji na vitongoji kujivika madaraka na kuvunja sheria za ardhi kwa kugawa ardhi kinyume cha sheria, hivyo kusababisha uvamizi kwenye maeneo yenye milki za watu wengine.

Dk. Mabula alitoa onyo hilo juzi wilayani Bagamoyo mkoani Pwani wakati akitoa na kukabidhi taarifa ya uchunguzi wa migogoro ya ardhi katika eneo la Mapinga

Taarifa hiyo iliyokabidhiwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, inatokana na kuundwa kwa kamati ya kuchunguza migogoro katika eneo hilo.

Katika taarifa yake ya uchunguzi, kamati ilibaini mambo 11 yaliyochangia uwapo wa migogoro katika eneo la Mapinga ikiwamo viongozi kujivika madaraka kinyume cha sheria kwa kugawa ardhi isivyo halali. Taarifa hiyo inaonyesha kuwa viongozi hao wamediriki kugawa hata maeneo yenye milki za watu na kusababisha migogoro.

Pia taarifa hiyo inaonyesha kuwa baadhi ya viongozi wamekuwa wakidiriki kughushi nyaraka au muhutasari wa ugawaji ardhi kwa kutumia majina ya viongozi wa zamani na kwa makusudi walishuhudia mauziano ya ardhi mara mbili katika ardhi moja kwa lengo la kujipatia fedha.

Pia kamati ilibaini kuwapo magenge ya uhalifu yanayovamia ardhi za wananchi na kutumia hila za kuanzisha mashauri mahakamani huku wakiendelea kuuza maeneo hayo jambo lililosababisha madhara makubwa katika utekelezaji wa uamuzi wa mahakama.

"Imebainika uwapo wa wavamizi kukimbilia kufungua mashauri mahakamani wakiwashtaki wamiliki halali wa ardhi lengo likiwa kuwazuia wamiliki kuingia kwenye maeneo yao huku wavamizi wakiendelea kuuza na kuendeleza maeneo hayo" alisema Waziri.

Dk. Mabula amemwelekeza Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Stela Tullo, kuanzia Septemba, mwaka huu, kufanya programu maalum ya kupunguza mlundikano wa mashauri ya ardhi katika wilaya ya Bagamoyo. "Watu hawa wanafahamika na kamati imewaorodhesha Mhe. Mkuu wa Mkoa nakukabidhi taarifa hii ili ushughulike na wote ambao wamekuwa wakikiuka maadili na kuvunja sheria kiasi cha kusababisha migogoro ambayo imekuwa ikileta maumivu makubwa kwa wananchi," alisema Dk. Mabula.

Hata hivyo , alisema baadhi ya migogoro ya ardhi katika eneo la Mapinga na maeneo mengine Bagamoyo imekuwa ikisababishwa na ununuzi wa ardhi unaofanywa haraka bila kujiridhisha umiliki halali wa eneo husika.

"Wanunuzi wananunua maeneo bila ya kufanya uhakiki katika ofisi za halmashauri lakini pale wanapogundua wametapeliwa ndipo huanza kupeleka malalamilo yao kwenye ofisi za serikali," alisema.

Dk. Mabula alitoa rai kwa wananchi wote wanaonunua ardhi kufanya uhakiki kabla ya kufikia hatua hiyo kupitia ofisi za halmashauri na kufanya upekuzi kujua miliki kuanzia ngazi ya halmashauri kwa yale maeneo yenye hati.

Pia alitahadharisha wananchi wanaovamia mashamba na kubainisha kuwa uamuzi wa serikali kushughulikia mashamba pori haina maana ya kuruhusu uvamizi na kusisitiza kuwa ni marufuku wananchi kuvamia maeneo hata kama ni shamba pori.

Pamoja na kamati iliyoundwa chini ya mwenyekiti Kamishna Msaidizi wa Polisi Peter Matagi kushughulikia migogoro ya ardhi ya eneo la Mapinga, iliwasikiliza wananchi wengine kutoka maeneo mbalimbali ndani ya Bagamoyo yakiwamo ya kata za Makurunge, Kidomole, Sanzale, Kerege, Mataya, Ukuni na Fukayosi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Kunenge alimweleza Waziri Mabula kuwa ataanza kuifanyia kazi taarifa hiyo kwa kuwashughulikia wote waliohusika bila kujali nyadhifa zao na kusisitiza kuwa hakuna mtu atakayeonewa wakati wa kushughulikia mgogoro huo.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akikabidhi taarifa ya uchunguzi wa migogoro ya ardhi katika eneo la Mapinga kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Alhaji Abubakar Kunenge, eneo la Mapinga, wilayani Bagamoyo juzi. **PICHA: WANMM**

# Wanaswa tuhuma kusababisha hasara ya mamilioni TANESCO

**Na Waandishi Wetu,** MWANZA

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) mkoani Mwanza limewakamata watu 16 kwa tuhuma za kuhujumu miundombinu ya shirika hilo na kulisababishia hasara ya Sh. milioni 18.

Watuhumiwa hao walikamatwa katika Wilaya za Magu, Nyamagana na Kwimba mkoani Mwanza katika msako uliofanywa jana na maofisa wa usalama wa TANESCO katika maeneo hayo walioshirikiana na Jeshi la Polisi.

Akizungumza baada ya kukamatwa kwa watuhumiwa hao Ofisa usalama wa shirika hilo, Jeverino Pembe alisema miongoni mwa watuhumiwa hao, wamo wafanyabiashara wa vyuma chakavu.

"Kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi tumewakamata watu wanaojihusisha na wizi pamoja na uharibifu wa miundombinu ya shirika letu na miongoni mwao ni mfanyabiashara wa vyuma chakavu," alisema na kumtaja kwa jina mfanyabiashara huyo.

Aliwataka wananchi wenye tabia za wizi wa nyaya za shaba katika transfoma, waache kufanya hivyo kwa kuwa ni kinyume cha kisheria na hatua hiyo inawapa hasara na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kutoa huduma za umeme katika maeneo mbalimbali.

**NEEMA YA EWURA**

Katika hatua nyingine, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Ziwa imetangaza neema kwa wafanyabiashara wanaotaka kujenga kituo cha mafuta vijijini kuwa sasa gharama zake ni Sh. milioni 40 hadi kukamilika kwake na kuanza kufanya kazi.

Meneja wa EWURA Kanda ya Ziwa, George Mhina, alisema katika mazungumzo na Nipashe jijini Mwanza kuwa kwa sasa kuanzia Sh. milioni 40 hadi Sh. milioni 50 mfanyabiashara anafungua kituo cha mafuta.

"Tumejikita katika kutoa elimu na tumetengeneza kanuni ndogo ambazo ni rafiki na ukiwa ukiwa na Sh. milioni 40 mpaka Sh. milioni 50 unaweza ukajenga kituo cha mafuta vijijini na wananchi wakapata huduma ya mafuta kutoka katika kituo cha mafuta ambacho bei imepangwa na EWURA na mafuta ambayo ni bora na salama kwa watumiaji," alisema.

"Sisi EWURA tunawapa taarifa zote muhimu ili watu waweze kupata tenda na kama kuna kampuni tutaisajili kwanza kwenye kanzidata yetu," alisema Mhina.

Katibu wa Kamati Ndogo ya Upimaji wa Tathmini ya Maonesho ya Sherehe za Wakulima Nanenane Kanda ya Ziwa Magharibi, Robert Samuel, alisema wametoa zawadi ya fedha taslimu, kombe pamoja na vyeti kwa washiriki waliofanya vizuri katika maonyesho ya Nanenane.

■**Imeandaliwa na Vitus Audax na Elizabeth Faustine (MWANZA)**

# Nchi 33 kujadili athari UVIKO-19

**Na Beatrice Shayo**

MKUTANO wa 13 wa Jumuiya ya Skauti wa Kike Tanzania (TGGA), utakaowaleta pamoja watu kutoka nchi 33 duniani, utafanyika nchini wiki ijayo kujadili mafunzo yaliyotokana na athari za janga la UVIKO - 19.

Sambamba na kujadili athari hizo, washiriki wataweka mikakati mipya kuwawezesha wasichana na wanawake kuwa rasilimali ya taifa utafanyika nchini wiki ijayo.

Kamshina Mkuu wa TGGA, Mary Richard, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo utakaoanza Agosti 22 hadi 26, mwaka huu

Alisema mwaka 2019 Tanzania iliibuka kuwa mshindi na mwenyeji wa mkutano huo na wanatarajia kuwa na zaidi ya watu 120 kwa kaulimbiu ya "Ustawi Pamoja: Rudisha Mustakabali wa Bara la Afrika kwa Kutumia Maarifa, Ujuzi na Vipaji vya Wanawake."

Richard alizitaja baadhi ya nchi zitakazoshiriki kuwa ni Angola, Burundi, Rwanda, Zimbambwe, Malawi, Uganda, Kenya, Madagascar, Afrika Kusini Nigeria, Ghana, Botswana, Burkina Faso, Cameroon, Chad, Congo, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Gambia, Guinea, Lesotho, Liberia, Mauritius, Namibia, Niger, Senegal, Sierra Leone, Sudani Kusini, Swaziland na Togo.

"Lengo la mkutano huu ni kutathmini hatua tulizopiga kwa miaka mitatu ya nyuma, tathmini ya changamoto na mafunzo yaliyotokana na janga la UVIKO - 19, kuweka mikakati mipya na kuchagua uongozi wa kipindi kingine cha miaka mitatu kuanzia sasa," alisema Richard.

Alisema mkutano huo ni nafasi ya kuona na kujifunza kutoka kwa nchi nyingine wanavyoendesha shughuli zao katika kukuza ufanisi na utendaji wa chama chao, na kwamba watatembelea vivutio mbalimbali.

Pia alisema TGGA malengo yake ni kumjengea mtoto wa kike maadili mema yatakayomwezesha kuwa rasilimali kwa taifa kwa kumpatia mafunzo ya vitendo yaliyo anje ya mfumo rasmi wa elimu.

Richard alisema TGGA ni mwanachama wa Chama cha Maskauti wa Kike Duniani (WAGGGS) chenye wanachama 150, Tanzania ikiwamo huku uwakilishi wa wasichana ukiwa ni milioni 10.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Rais Samia kutenga chumba cha malezi watoto sokoni, muhimu

**JUZI** wakati Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa mkoani Njombe kwenye uzinduzi wa soko kuu mkoani humo, alimwagiza Mkuu wa Mkoa huo, Antony Mtaka, kuhakikisha soko linatenga chumba kwa ajili ya watoto ambao mama zao wanafanya biashara zao katika soko hilo.

Agizo hilo la Rais lilitokana na kushuhudia kinamama wengi wafanyabiashara, wakifanya shughuli zao huku wakiwa wamebeba watoto wao mgongoni.

Rais Samia, alisema kitendo hicho sio tu kinawaathiri watoto, bali hata wazazi wao ambao baadaye wanaweza kupata madhara katika miili yao.

Akizungumza katika ufunguzi huo, Rais Samia alisema ameona kinamama wengi wamebeba watoto migongoni na kushauri itakuwa vizuri wakamegewa sehemu ya soko hilo wakaweka eneo la kuangalia watoto ili wakati mama yupo kazini na biashara zake watoto hao wawe wanashughulikiwa mahala pazuri, wanapata chakula vizuri, wanakua vizuri, wanapata elimu huku wanatunzwa vizuri.

Alimwagiza Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kuangalia nafasi nzuri kwa ajili ya watoto hao.

Agizo hilo la Rais limekuja wakati mwafaka kutokana na kinamama wengi wafanyabiashara iwe ya sokoni, mamalishe au kutembeza bidhaa barabarani, kutembea na watoto wao kwenye shughuli zao, pengine wanafanya hivyo kwa kukosa msaada wa kulea watoto hao nyumbani.

Athari za watoto kuambatana na wazazi sehemu za biashara ni watoto kuiga tabia ambazo haziendani na umri wao.

Tumeshuhudia sehemu zenye mikusanyiko ya watu hasa sokoni, kuna watu wenye tabia tofauti kwa kutoa lugha na vitendo vizisivyofaa bila kujali kuna watoto.

Pia, watoto wanapata mateso ya kukosa haki yao ya kucheza na kupata elimu kutokana na muda mwingi kuambatana na mama zao kwenye shughuli zao za biashara.

Watoto hao pia wanakuwa katika mazingira hatarishi kwa sababu maeneo ambayo wanawekwa wakati wazazi wao wakiendelea na shughuli sio rafiki kwao.

Agizo la Rais la kutaka maeneo ya soko kutengwa vyumba maalumu vya kutunzia watoto hao, litasaidia kupata haki yao ya kufurahia uhuru wao kucheza na watoto wenzao, kupata matunzo mazuri na pia kupata chakula kizuri, kama alivyopendekeza Rais.


Mtoto anapozoea mazingira yasiyoendana na umri wake, kwa vyovyote anabeba tabia anazoziona kila siku na kukua nazo, na inapotokea kuwa ni mbaya matokeo yake ni kuwa mtoto mwenye tabia mbaya.

Unaweza kukuta mtoto anatoa matamshi au vitendo ambavyo haviendani na umri wake kwasababu tu amezoea kusikia wakubwa wakitamka na kwake kuona ni sawa.

Ni vizuri maeneo ambayo wajasiriamli kinamama wanaokosa msaada wa malezi kwa watoto wao majumbani mwao, wakajengewa vituo vitakavyowasaidia watoto wao kuondokana na athari zitakazoathiri maisha yao ya baadaye.

Ni matumaini yetu kuwa agizo lililotolewa na Rais Samia, litakuwa chachu kwa maeneo yote ambayo wafanyabiashara kinamama, watatengewa eneo la kuweka watoto wao na mwalimu atayewasaidia kuwapa elimu na kukua katika malezi mema na mazingira mazuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Mkakati kuinua wazee uje na matokeo chanya

Na Sabato Kasika

**LENGO** namba moja la Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ni kutokomeza umaskini wa aina zote kwa kila mtu na kila mahali, ili kuongeza kipato cha watu waishio katika hali duni na kuwapatia huduma za msingi.

Maelekezo ya lengo hilo yanazitaka serikali kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, zimetokomeza umaskini uliokithiri kwa wanaoishi kwa kipato chini ya dola 1.25 (kwa siku) aidha, idadi ya wanaume, wanawake na watoto wa kila umri wanaoishi katika hali ya umaskini inapungua angalau, kwa kuwa wote wana haki sawa za kiuchumi na upatikanaji wa huduma za msingi.

Kadhalika, serikali inatakiwa kutambua wananchi wanaoishi katika umaskini, ili kuelekeza rasilimali na huduma kwao, kwa ajili ya kuwasaidia kuepuka hali hiyo na kuwajengea uwezo watu maskini na kuwaimarisha.

Katika kufanikishaa lengo hilo, Tanzania, haijabaki nyuma, kutokana na uamuzi wake wa kukusudia kuwekeza katika makazi ya wazee ili kuwa na miradi mbalimbali itakayozalisha mazao na kuchangia katika mapato ya serikali.

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zanaib Chaula, anasema anapozungumza na wana habari baada ya kuzungukia makazi mbalimbali ya wazee.

> **Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zanaib Chaula, anasema anapozungumza na wana habari baada ya kuzungukia makazi mbalimbali ya wazee.**

Anasema kuna makazi 14 nchini yanayosimamiwa na serikali, ili kuweka mikakati na mbinu mbalimbali zitakazosaidia makazi hayo kuwa na huduma bora na kuwekeza nguvu katika miradi ya kilimo, mifugo na uzalishaji mali katika makazi hayo.

Miongoni mwa makazi hayo ni Nunge Dar es Salaam, Kolandoto Shinyanga, Njoro Kilimanjaro, Magugu Manyara, Kiilima Kagera, Fungafunga Morogoro na Sukamahela Singida. Ninaamini kuwa, uwekezaji wa miradi ya maendeleo katika makazi ya wazee ni hatua nzuri, kwani itaipunguzia serikali baadhi ya gharama zikiwamo za chakula.

Kwa mfano, inaelezwa kuwa baadhi ya makazi ya wazee yana ekari 10 ambazo zinaweza kutumika kwa shughuli za kilimo cha mboga, ufugaji wa kuku na miradi mingine ya kimkakati.

Iwapo kilichukusudiwa na serikali kitatimia, ni wazi kila makazi yanaweza kuinuka kiuchumi na hata kusaidia wazee kuwa na afya bora inayotokana na vyakula na mboga ambazo zitakuwa zinalimwa katika makazi hayo.

Lengo hilo namba moja halitaki mtu kuachwa nyuma kiuchumi, kwani linataka kuwapo kwa matokeo chanya kwa wote, hapo ndipo unapokuja umuhimu wa kuboresha makazi ya wazee kwa kuyaanzisha miradi.

Nakumbuka katika bajeti ya mwaka 2021/2022, Wizara ya Afya ilitenga Shilingi bilioni 7.4, kwa ajili ya kuboresha makazi ya wazee taarifa ya Waziri Dk. Dorothy Gwajima alioiwasilisha mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ilisema kuwa huduma za chakula na mahitaji ya msingi vimeboreshwa.

Kwamba uboreshwaji huo umekwenda sambasamba na kuanzisha miradi ya bustani na ufugaji ambayo hutekelezwa na kusimamiwa na wazee wenyewe, hatua ambayo inaweza kuinua uchumi wao.

Anaeleza kuwa katika makazi hayo 14 yanayohudumiwa na serikali, kuna watumishi 93 wa kada mbalimbali na 19 kati yao maofisa ustawi wa jamii, ambao wanashauriwa kuwa wabunifu wa miradi katika makazi hayo.

Lakini pamoja na juhudi hizo kuinua uchumi wa makazi ya wazee, ingekuwa vyema iwapo jamii itawajibika katika malezi ya wazee, kwa kuwa sehemu salama na ya kwanza ya wazee ni katika familia zao.

Ninaamini kuwa wazee wanaweza kupata huduma bora na uangalizi mzuri kutoka kwa ndugu na familia zao, suala la kupelekwa katika makazi ya wazee iwe ni ya mwisho baada ya kukosekana wa kuwalea.

## Mshtakiwa aomba mashahidi kutoa ushahidi upya dhidi yake

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA anayedaiwa kutoroka, Pepetua Ngondwe, ameomba mashahidi wote ambao walitoa ushahidi wakati hayupo, watoe upya ushahidi wao ili ajue wanamtuhumu kwa kitu gani.

Kutokana na maombi hayo, Mhakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeruhusu shauri hilo lianze upya na mashahidi sita waliotoa ushahidi, watoe ushahidi wao upya.

Uamuzi huo ulitolewa na Hakimu kazi Mkuu Huruma Shaidi, baada ya kusikiliza maombi ya mshtakiwa ambaye anataka kuwasikiliza mashahidi hao ili ajue anatuhumiwa na kitu gani na pia hawafahamu.

"Naiomba Mahakama mashahidi waliotoa ushahidi dhidi yangu warudie kwa sababu wakati wanatoa ushahidi mimi sikuwapo mahakamani," alidai Ngondwe.

Baada ya mshtakiwa kudai hayo, Hakimu Shaidi akamuuliza wewe si ulikimbia? Alijibu kwamba hakukikimbia alikuwa anaumwa.

Wakili wa Serikali, Adolf Lema, alidai mashahidi waliotoa ushahidi ni sita na wakati wakifanya hivyo, mshtakiwa hakuwapo na pia mashahidi hao walilipwa gharama zote.

Lema alidai kwamba mshtakiwa aseme anataka shahidi gani ili kuokoa fedha zinazotolewa na mahakama na pia anataka nini cha kuuliza kwa sababu mashahidi walikuwa sita.

"Sheria inaruhusu mashahidi kutoa ushahidi bila mshtakiwa kuwapo. Hata hivyo, angeisaidia mahakama anataka mashahidi gani na nini anachokitaka japokuwa alitoroka lakini anayo haki ya kusikiliza mashahidi," alidai Lema.

Baada ya hoja hizo, Ngondwe alidai kati ya mashahidi sita, anawataka watatu akiwamo mlalamikaji, Ritha Lemi.

Akitoa uamuzi wa hoja hizo, Hakimu Shaidi alisema pamoja na ukweli kwamba alitoroka na kesi ikaendelea kusikilizwa kwa mujibu wa sheria hadi alipokamatwa, mashahidi wote sita walitoa ushahidi wakati hayupo.

"Kila mtu ana haki ya kusikilizwa hivyo pamoja na kusema unataka mashahidi watatu, baadaye hukumu itakapotolewa utasema hukutendewa haki utakata rufaa (rufani).

"Naomba shauri lianze upya na mashahidi wote wameanza upya kutoa ushahidi, hivyo wiki hii wajipange shauri lianze kusikilizwa. Kesi imeahirishwa hadi Agosti 18, mwaka huu," alisema.

Ngondwe anatuhumiwa kujipatia zaidi ya Sh. milioni 315 kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa Ritha Lemi.

# Watanzania kupatiwa vyeti vya kuzaliwa ifikapo 2030

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema hadi mwaka 2030 serikali itakuwa imefikia malengo ya Watanzania wote kusajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Alisema hayo jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Usajili wa Matukio Muhimu kwa Binadamu ambayo kitaifa yalifanyika Dar es Salaam.

"Rais (Samia Suluhu Hassan) ametuelekeza ifikapo mwaka 2025 watoto wote nchini chini ya umri wa miaka 18, wawe wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa na ikifika mwaka 2030 lazima Watanzania wote wawe wana vyeti vya kusajiliwa, wana vyeti vya ndoa, au vyeti vya talaka pale inapohitajika," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema kuanzia Januari, mwakani, kila kituo cha afya, zahanati au hospitali ya wilaya lazima itoe cheti cha usajili na cheti cha kuzaliwa hapo hapo.

Pia alisema kila mtoto anayekwenda shuleni atatakiwa kuwa na cheti cha kuzaliwa na kwa wale wasiokuwa navyo watasajiliwa katika shule husika na kupatiwa vyeti hivyo.

"Na maagizo ya Rais ni kwamba kuanzia Januari, mwaka kesho, kila mtoto anayekwenda shuleni anatakiwa awe au cheti cha kuzaliwa au asajiliwe pale pale shuleni anapokwenda. Kwa hiyo kuanzia chekechea, shule ya msingi, sekondari na vyuo usajili unakwenda sambamba na usajili wa taasisi husika ya elimu," alisema.

Pia, alisema kuanzia sasa mpaka mwaka 2030 wanataka Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ijiendeshe kidijitali.

"Katika kutekeleza maazimio na maelekezo ya Rais, tunataka RITA iwe ya kidijitali, tunataka takwimu zote zinazokusanywa kutoka shuleni, hospitali na kwa wananchi wa kawaida, zipelekwe katika wakala huu kidijitali na tunataka kumfikia mwananchi pale alipo katika kila kona ya nchi hii," alisisitiza.

Dk. Ndumbaro alisema kwa sasa wanaunganisha mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na ya TAMISEMI ili kuhakikisha Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) inatekeleza kwa urahisi majukumu yake.

"Tunataka takwimu za RITA, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na za anwani ya makazi, zisomane na tukifanikisha mifumo hiyo na ile ya utoaji haki na ya taasisi za fedha kwa ajili ya mikopo, ajira, mirathi na mingine yote, itakuwa rahisi kwa mwananchi kupata huduma," alisema Dk. Ndumbaro.

"Ili kufanikisha hilo, ni lazima turudi kwenye vitongoji na mitaa na vijiji. Tumekubaliana na mawaziri shirika kwamba katika kila kata ni lazima kuwe na ofisi kwa ajili ya usajili kwa watoto wanaozaliwa Tanzania.

"Katika mradi wa kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano unakwenda vizuri sana, mwaka 2012 kabla ya kuanza kwa mradi huo, watoto waliokuwa wamesajiliwa walikuwa asilimia 13, lakini mpaka mwaka huu watoto waliosajiliwa ni asilimia 65," alisema.

Kabidhi Wasii Mkuu na Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Angela Anatory, alisema bado kunahitajika ushiriki wa wadau mbalimbali kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa huduma kwa wakala huyo.

Naye mwakilishi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Ousmane Niang, aliipongeza RITA kwa kuanzisha mfumo wa kusajili watoto walio chini ya miaka mitano katika maeneo yao wanayoishi.

Pia, alisema ni muhimu nchi za Afrika kuweka mkazo kwenye masuala hayo ya usajili matukio muhimu na kwamba katika kufanikisha hilo kunahitaji utashi wa kisiasa.

Mwakilishi kutoka Ubalozi wa Canada, Helen Fytche, alisema nchi hiyo inathamini katika mchango wa kila mtu katika nchi kuhesabiwa na kwamba hadi sasa nchi hiyo imesaidia kuimarisha mifumo ya usajili kwa kutoa Sh.bilioni 55 tangu mwaka 2015.



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wakifanya maboresho ya miundombinu ya maji katika eneo la Majohe, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Jafo ataka vibali ujenzi, ramani kuzingatia utunzaji wa mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ameagiza ugawaji ramani na vibali vya ujenzi kwenye Halmashauri nchini uzingatie idadi ya upandaji miti na utunzaji wa mazingira.

Pia amesema upandaji wa bei za bidhaa hasa za chakula unaotokana na kuwapo kwa uzalishaji mdogo wa mazao unasababishwa na kufanyika kwa shughuli za kibinadamu ambazo si rafiki wa mazingira.

Akizindua jana kampeni ya Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) na Mazingira, inayolenga kupandwa miti 540 katika eneo la Ipagala kati ya 2,000 itakayopandwa Dodoma, Jafo alisema wakurugenzi wa halmashauri wanapogawa viwanja lazima waonyeshe kwenye ramani miti mingapi inapaswa kupandwa.

"Kama kila kiwanja kilichopimwa kikiwa kinapanda walau miti mitatu kama vya hapa maeneo yetu yatakuwa ya kijani na haya ni maelekezo yangu kwa Wakurugenzi wote kwamba Building permit lazima ziendane na ajenda ya utunzaji mazingira katika nchi yetu," alisema.

Pia alisema tathmini iliyofanyika hivi karibuni imeonesha lengo la upandaji miti milioni 276 kila mwaka, kwa kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5, limefikia asilimia 80 ya utekelezaji.

Alitaka miti hiyo iliyopandwa kutunzwa ili isiliwe na ng'ombe na kutoa siku 14 kwa Shirika hilo kujenga uzio na kuweka geti kwenye eneo hilo.

"Dodoma ni Mkoa ng'ombe pekee ambao utakuta ng'ombe wanatembea barabarani wekeni uzio ili kulinda hii miti msipoitunza maana yake yote italiwa na ng'ombe,"alisema.

Waziri huyo aliziomba taasisi nyingine nchini kuendelea kuiga kilichofanywa na Stamico ili kutunza mazingira kwa kuwa suala hilo ni jukumu la kila mmoja. Dk. Jafo alitoa wito kwa watanzania kuhakikisha kila kaya inapanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo ni janga kwa dunia.

Naye, Waziri wa Madini, Dk.Doto Biteko, alisema wizara hiyo itahakikisha inasimamia ajenda ya mazingira kwenye shughuli za uchimbaji madini.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, alisema kampeni hiyo inalenga kuhifadhi mazingira na uoto wa asili.

"STAMICO tunazuia ukataji miti kwa kupanda miti na kuhamasisha matumizi ya mkaa mbadala ambapo kampeni hii itazinduliwa kesho(leo) rasmi na lengo letu ni kupanda miti 10,000 ambapo 2,000 itapandwa Dodoma na mingine 8,000 maeneo ambayo Stamico ina miradi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alishauri Wizara ya Madini kutafuta njia ambayo ni rafiki kwa uhifadhi wa mazingira ili kuepuka kuchoma miti.

# CCM yaagiza utambuzi vyanzo vya maji nchini

**Na Mary Geofrey,** LUSHOTO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amemwagiza Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kuvitambua na kuviwekea mipaka vyanzo vya maji nchini.

Chongolo alitoa agizo hilo jana alipozungumza na wanachama wa CCM wilayani Lushoto mkoani Tanga katika ziara yake kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo na kuhimiza ushiriki wa wananchi katika Sensa ya Watu na Makazi iliyopangwa kufanyika mwezi huu.

Alisema wizara inatakiwa kuvitambua vyanzo hivyo vya maji ili kudhibiti watu wanaovivamia na kufanya shughuli za kilimo na ufugaji na kusababisha tatizo la ukosefu wa maji.

"Ninaiagiza Wizara ya Maji ianze mpango maalum wa haraka wa kuvitambua vyanzo vyote vya maji na kama vinamilikiwa na wananchi, vichukuweni na kuwekewa mipaka kama ilivyo kwa TANROADS (Wakala wa Barabara Tanzania) wana alama za mipaka ya barabara na wanazitambua," aliagiza.

Chongolo pia alisema wazee wa zamani walikuwa wakitunza vyanzo vya maji na ndiyo sababu hadi sasa vipo na vinatumiwa na watu.

"Maji ni uhai, kila mtu anahitaji maji, nimeona baadhi ya maeneo watu wanachezea vyanzo vya maji, siyo sawa, hivi vyanzo vinahitaji kutunzwa vyema kwa ajili ya manufaa yetu," alisisitiza.

Chongolo pia aliuagiza uongozi wa mkoa huo kusambaza miche milioni tano ya kahawa kwa wananchi ili kufufua zao hilo.

Alisema awali mkoa huo ulikuwa ukizalisha tani 300 za kahawa lakini kwa sasa hawazalishi tena, hivyo kuwataka kufufua zao hilo ili kuongeza idadi ya mazao ya biashara wanayozalisha na kukuza uchumi wa mkoa huo.

Akiwa katika Halmashauri ya Bumbuli, Chongolo aliwahimiza wazazi na walezi kuepuka kukatisha masomo watoto wa kike kwa lengo la kuwaozesha.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Said Mgumba, aliahidi kuiinua Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli kimapato kutoka kushika nafasi ya mwisho kwenye makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri nchini.

Aliahidi kuwa atatumia mbinu alizotumia katika Halmashauri ya Ileje na Tunduma mkoani Songwe, ambazo awali zilikuwa zina makusanyo kidogo.

Mgumba ambaye awali alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe kabla ya kuhamishiwa Tanga, alitoa ahadi hiyo jana mbele ya Chongolo.

"Wilaya ya Tunduma ilikuwa inakusanya Sh. bilioni 5.2 lakini mpaka sasa inakusanya Sh. bilioni 8.5, ndani ya mwezi mmoja kabla ya kuondoka Julai 30, Sh. bilioni 1.044, maana yake ni nini? Mambo yanawezekana na hapa Bumbuli yatawezekana, ninakuahidi Katibu Mkuu, tutaondoka katika hatua hii ya mwisho," aliahidi Mgumba.

Chongolo alipongeza kiongozi huyo kwa juhudi zake za kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kwenye kusimamia mkoa huo hasa kwa kuahidi kuongeza mapato.




Meneja wa Bidhaa na Vifaa vya Intaneti wa Tigo, Imelda Edward, akizungumza katika uzinduzi wa promosheni iitwayo "Kali kuliko", jijini Dar es Salaam jana, ambapo mteja atakaponunua simu janja aina ya Infinix NOTE 12 na HOT 12 series, atajishindia zawadi mbalimbali. Kulia ni Meneja Mauzo wa Infinix, Jackline Steven. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakala Songesha yawaongeza ari mawakala

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Vodacom Tanzania, imeanzisha huduma mpya za mikopo kwa mawakala kwa lengo la kukuza mitaji yao na kuendelea kuwahudumia wateja hata wanapoishiwa salio kwenye akaunti zao.

Meneja Masoko wa M-pesa, Noel Mazoya, alisema jana kuwa huduma hiyo itawapa mawakala fursa ya kukopa mtaji hadi Sh. Milioni sita, hivyo kumaliza tatizo la mawakala kushindwa kuwahudumia wateja kwa kukosa salio.

Akizungumza wakati wa hafla ya kutambulisha huduma hiyo kwa mawakala wa M-Pesa mkoa wa Mwanza, Mazoya alisema kupitia elimu kwa wateja inayoenda kwa jina la Wakala Ticha, mawakala wa M-Pesa watajiingizia kipato kulingana na idadi ya wateja watakaowaelimisha na kujiunga na huduma mbalimbali.

"Kampuni ya Vodacom pia imeongeza kamisheni kwa mawakala huku ikipunguza tozo ya kutuma na kutoa fedha kwa wateja wa M-Pesa," alisema Mazoya. Alisema kupitia kampeni ya M-Pesa Imeitika, kampuni imetenga zaidi ya Sh. milioni 350 kwa ajili ya zawadi ya fedha taslimu, bajaji, pikipiki, kuponi ya kujaza mafuta tangi zima na nyumba yenye samani zitakazotolewa kwa mawakala na wateja wa huduma ya M-Pesa.

"Kupitia kampeni yetu iliyoanza Julai 6 na kutarajiwa kukamilika Septemba 6, mawakala na wateja wa M-Pesa watajinyakulia zawadi ya fedha taslimu kila siku, bodaboda nne na bajaji moja kila wiki, ofa ya kujaza mafuta na zawadi kuu ikiwa ni nyumba yenye samani zote katika droo kubwa.

"Vodacom imewekeza zaidi katika kuwawezesha mawakala kwa sababu licha ya kuwa injini ya huduma ya M-Pesa, pia ni eneo linalotoa fursa za ajira kwa vijana kutokana na zaidi ya watu 150,000 kujiajiri moja kwa moja kupitia huduma hiyo huku mnyororo wake wa thamani ukinufaisha zaidi ya watu milioni moja," alisema.

Victoria Chale, Meneja Mauzo Mwandamizi wa Vodacom Kanda ya Victoria, inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita na Mara, aliwataka mawakala, hasa wanawake ambao awali walikabiliwa na tatizo la mitaji kutumia huduma mpya ya Wakala Songesha kukuza mitaji yao.

Wakala Mkuu wa M-Pesa eneo la Soko la Pasiansi jijini Mwanza, Salum Rweyagaza, aliishukuru Vodacom kwa kubuni huduma ya Wakala Songesha akisema imemaliza tatizo la kupunguki-wa salio lililokuwa linawakabili mawakala, hasa wenye mitaji midogo.

"Kwa sasa ninaweza kukopa mtaji hadi Sh. milioni sita na kuendelea kuwahudumia wateja kwa riba ndogo ya asilimia 10. Huduma hii ni ukombozi kwetu mawakala," alisema.

# Mbegu 141 za asili kuboreshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imetaja vipaumbele sita vya mwaka 2022/23, ikiwamo kuzifanyia utafiti na kuziboresha aina 141 za mbegu mbalimbali za asili.

Pia TARI imepanga kuzalisha teknolojia mpya ikiwamo mbegu zenye sifa zaidi ya zile zinazotumiwa kwa sasa ili kutoa mavuno mengi kwa wakulima.

Meneja wa Mawasiliano na Menejimenti ya Maabara wa TARI, Dk. Richard Kasuga, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema utafiti wa mbegu za asili utaongeza wigo katika kukidhi mahitaji ya soko na kilimo cha biashara kwa kushirikiana na viwanda pamoja na wafanyabiashara.

"TARI imepanga kuzalisha teknolojia mpya zikiwemo aina za mbegu zenye sifa zaidi ya zile zinazotumiwa kwa sasa. Aina hizo za mbegu zina sifa ya kutoa mavuno mengi, kustahimili ukame, ukinzani dhidi ya magonjwa na wadudu, zenye viinilishe vingi, pamoja na sifa zingine za soko kama vile sifa za mezani," alisema.

Dk. Kasuga alibainisha kuwa teknolojia zingine zitakazogunduliwa ni za uongezaji thamani katika mnyororo wa thamani wa mazao, kuboresha afya ya udongo, kugundua mbinu bora za ukuzaji mazao, zana bora za kilimo, na utunzaji wa mazao baada ya mavuno.

"Katika mwaka wa fedha wa 2022/23 teknolojia 35 zitazalishwa. Kati ya hizo 15 ni mbegu bora, tano agronomia, tano afya ya udongo na 10 teknolojia baada ya mavuno," alisema.

Pia alisema alisema wakulima 5,000 na maofisa ugani 500 watapatiwa mafunzo ya kilimo bora cha mazao mbalimbali na Wasindikaji Milioni mbili watapatiwa teknolojia mpya za kuongeza thamani ya mazao.

Dk. Kasuga alisema pia miche na pingili zipatazo milioni 50 ya mazao mbalimbali ambayo ni parachichi, mkonge, michikichi, minazi, mihogo, viazi vitamu na ndizi itazalishwa na kusambazwa kwa wakulima kwa kipindi hicho.

Kuhusu umwagiliaji, alisema TARI imetengewa fedha za kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika eneo la hekta 854 kwenye vituo 15 vya utafiti wa kilimo. Alisema taasisi imepanga kuboresha maabara ya udongo katika kituo cha TARI Mlingano ili kupata ithibati ya kimataifa.

Meneja huyo alisema matarajio ya vipaumbele hivyo ni kuongeza wakulima watakaopokea teknolojia kutoka asilimia 34.2 hadi asilimia 50.

"Pia uzalishaji wa mazao utaongezeka kutoka tani 1.5 hadi tani 4.0 kwa hekta kwa zao la mahindi, tani 2.3 hadi tani 4.5 kwa hekta kwa zao la mpunga na tani 1.3 hadi tani 2 kwa hekta kwa zao la mtama. Vilevile zalishaji wa alizeti utaongezeka kutoka tani moja hadi tani mbili kwa hekta,"alisema.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Makutupora, Dk. Cornel Massawe, alisema taasisi hiyo imeagiza aina nne za mbegu ya zabibu kutoka nchini Afrika Kusini zinazosifika kwa ubora ili kuzifanyia utafiti na zitumike kuzalishwa nchini.

## Aliyejitoa uchaguzi CCM ashinda

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KATIKA hali iliyowashangaza wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi ya Kata ya Kilago, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ni mgombea wa kiti cha Katibu wa Itikadi na Uenezi kujitoa kugombea nafasi hiyo na kushinda nafasi hiyo bila kuwapo katika uchaguzi.

Mgombea huyo, Peter Madalali ambaye awali alichukua fomu ya kugombea ngazi ya kiti hicho na kuamua kujitoa kutokana na sababu za kifamilia, alijikuta akishinda bila ya kuwapo hali iliyozua taharuki katika uchaguzi.

Akizungumza na gazeti hili baada ya uchaguzi huo, Madalali alisema, alichukua fomu kwa ajili ya kugombea kiti hicho, lakini baada ya kuwapo kwa matatizo ya kifamilia aliamua kujitoa kugombea na kufanya idadi ya wagombea kuwa watatu.

Alidai kuwa, alipigiwa simu na wajumbe wa uchaguzi huo na kuambiwa jina lake limerejeshwa na kutakiwa kufika kuomba kura mbele ya wajumbe hao na waliompigia simu walikuwa na mgombea wao tayari wamemwandaa, lakini jina lake lilikatwa katika vikao vya juu na kurejeshwa.

Aidha, alisema alipofika kuomba kura wajumbe wa uchaguzi huo walimkataa kwa sababu tayari alikuwa ameandika barua ya kujiondoa kushiriki uchaguzi hali iliyomfanya kuondoka katika eneo la uchaguzi ili kuendelea na mambo mengine.

"Mimi nilichukua fomu na kujaza kwa ajili ya kugombea nafasi hii, lakini baada ya kuwa na matatizo ya kifamilia niliamua kujitoa kugombea kwa kuandika barua, lakini jina langu limerejeshwa na nimeomba kura na wajumbe wamenikataa na nimeuamua kuondoka," alisema Madalali.

Kwa upande wake Katibu wa CCM Wilaya ya Kahama, Mary Mhoha alisema, mtu akishachukua fomu ya kugombea nafasi yoyote, kuijaza na kuirejesha baadaye akaandika barua ya kujiengua katika uchaguzi chama kinakuwa kinaamini ni mgombea halali isipokuwa kama atachukua fomu akairejesha bila kujaza anakuwa amejiondoa kihalali.

Baada ya kauli hiyo, wajumbe waliamua kupiga kura hizo na kufanya mgombea aliyeandika barua ya kujitoa katika uchaguzi kushinda kiti hicho huku akiwa hayupo katika eneo hilo hali iliyozua taharuki kwa wanachama ya kutaka kupigana.

Naye diwani wa kata hiyo, Charles Masele alisema, uchaguzi ndani ya chama umekwisha salama na walishindwa kupata nafasi mbalimbali zilizokuwapo wajipange katika awamu nyingine baada ya miaka mitano ijayo na kuwasihi kushirikiana na kuvunja makundi.

Katika uchaguzi huo wagombea wote waliokuwa wakigombea nafasi mbalimbali walipita bila ya kupingwa isipokuwa nafasi ya Katibu wa Itikadi na Uenezi ambayo uchaguzi ulileta shida, lakini uliisha salama na kumkubali kuwa kiongozi wao.

# Serikali yakusudia kusitisha uwekezaji Ziwa Babati

**Na Mbaraka Kambona**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki na Waziri wa Nchi-Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, wanakusudia kusitisha uwekezaji uliofanywa katika Ziwa Babati na kampuni ya watu wa China ya XIN SI LIU baada ya kuonekana dosari kadhaa zilizoainishwa na mamlaka zilizo chini ya wizara hizo.

Mawaziri hao walibainisha hilo juzi mkoani Manyara wakati wa mkutano wa majumuisho baada ya kwenda kutembelea eneo linalokusudiwa kuwekwa mradi huo na kupokea taarifa kutoka kwenye mamlaka zilizokuwa zikifanya tathmini ya uwekezaji huo.

Akizungumza juu ya aina ya uwekezaji uliotarajiwa kufanyika katika eneo hilo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema kwa mujibu wa taarifa waliyopokea na hali waliyoiona ufugaji wa samaki kwenye vizimba kwenye eneo hilo la ziwa hauwezi kuwa na matokeo chanya kwa mwekezaji na utasababisha mgogoro baina ya wananchi na serikali na kushauri mwekezaji huyo kuangalia eneo jingine ambalo anaweza kufanya uwekezaji wenye faida kwake na tija kwa taifa kwa ujumla.

"Kwenye rasilimali yoyote ni lazima yaangaliwe maslahi ya pande zote mbili ambayo ni upande wa mwekezaji na upande wa wanufaika wa wadau wanaozunguka eneo la uwekezaji na kazi yetu kama serikali ni kupima na kuangalia uzito uko wapi zaidi," alisema.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, alisema kuwa taarifa iliyotolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), imeainisha athari za kimazingira zitakazotokea kwa upande wa Ziwa Babati kutokana na uwekezaji huo ambao aliwataka wataalamu kuendelea kuwashauri wawekezaji usahihi na usalama wa maeneo wanayokusudia kuwekeza.

Awali, akipendekeza kusitishwa kwa uwekezaji huo Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, Pauline Gekul, alisema kuwa uwekezaji huo utaibua migogoro kwa wananchi wa wilaya hiyo hasa kutokana na ziwa hilo kutegemewa na zaidi ya wavuvi 1000 kuendesha maisha yao.

Kampuni ya China ya XIN SI LU ilikuwa inakusudia kufanya uwekezaji wa ufugaji wa samaki kwenye vizimba katikati ya Ziwa Babati na ilitarajia kuchukua eneo la ukubwa wa hekari tatu kwa ajili ya shughuli hiyo jambo ambalo limeonekana kuwa na athari ya mazingira na kiuchumi kwa wananchi wanaonufaika na ziwa hilo.



Mtaalamu wa Programu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Dk. Mariam Ngaeje (kushoto), akielezea shughuli za shirika hilo, kwenye warsha ya waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani inayofikia kilele chake leo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Jamii yakumbushwa kuwajali wazee

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

KATIBU Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainabu Chaula, ameitaka jamii kuacha tabia ya kuwatelekeza wazee na ijikite kuwapatia mahitaji muhimu ikiwamo matibabu na huduma nyingine za kijamii.

Dk. Zainabu aliyasema hayo juzi mkoani Morogoro alipotembelea makazi ya wazee ya Fungafunga yaliyoko Manispaa ya Morogoro na kwamba wajibu wa kuwathamini na kuwatunza wazee ni jukumu la kila mmoja katika jamii.

"Wajibu wa kuwatunza na kuwathamini wazee katika jamii zinazotuzunguka ni jukumu la kila mtu hivyo natumia nafasi hii kuwasisitiza wananchi wa mkoa huu na kwingineko nchini kuhakikisha wazee wetu wanathaminiwa," alisema Zainabu.

Alisema kuwatunza na kuwathamini ni jambo la busara ambalo kila mtu anatakiwa kulifanya na kuacha tabia ya kuwadhihaki, kuwanyanyapaa na kwamba kila mtu anatakiwa huhakikisha kundi hilo linapata matunzo mazuri.

Kadhalika, alisema amekuwa akiguswa na kitendo cha wazee kuthamini na kuikumbusha jamii kuwa uungwana wa mtu hupimwa kwa matendo mazuri na sio kwa maneno pekee na kutaka kutambua hilo.

Hosea Mganga ni miongoni mwa wazee 21 wanaolelewa kituo cha Fungafunga ambaye ameiomba serikali kuitazama miundombinu yote ya usafiri inayozunguka katika kituo chao hicho.

Mzee Mganga alisema barabara ya kufika kituoni hapo kuna daraja ambalo halina ubora na kwamba kituo kikipata hitilafu ya umeme watu wa TANESCO au Zimamoto itakuwa vigumu kufika kwa urahisi na kuiomba serikali iitazame suala hilo kwa jito la tatu.

"Tunaishukuru serikali kwa malezi inayotupatia ila tunaomba pia iboreshe miundombinu ya usafiri ili wakati wa dharura inapotokea huduma ya usafiri hasa wa gari isilete usumbufu wa kutofikika kwa urahisi katika kituo hiki cha Fungafunga," alisema Mganga.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Wazee Taifa, Lameck Sendo, alisema mikakati waliyonayo kwa sasa ni kuhakikisha wazee wanapata mahitaji stahiki maeneo mbalimbali kwenye jamii zinazowazunguka nchini.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa hiyo, Rehema Kombe, alisema mkakati uliopo ni kuboresha kituo hicho na kwamba zoezi hilo litaanza kutekelezwa hivi karibuni ili kuhakikisha mazingira yote ya kituo hicho yanakuwa rafiki zaidi kwa wazee hao.

# TAKUKURU yabaini 'madudu' kwenye ujenzi wa madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, imebaini kuwapo dosari kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa kutokana na kuta kupinda.

Mkuu wa TAKUKURU, Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy, alibainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu utendaji wa kazi kwa mwaka wa fedha (2021-2022), kuanzia Aprili hadi Juni.

Alisema katika uzuiaji wa rushwa walifanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za UVIKO-19 kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo 17 yenye thamani ya Sh. bilioni 13.7, ikiwamo wa vyumba vya madarasa na kubaini kujengwa chini ya kiwango na kuta kupinda.

"Miradi ya maendeleo ambayo tulifuatilia ya fedha za UVIKO-19 ni katika Sekta ya Elimu, Maji, Afya na Utawala, na kati ya miradi yote 17, minne tuliikuta ina dosari kwa kujengwa chini ya kiwango," alisema Kessy. "Kwa upande wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Halmashauri ya Msalala na Ushetu, wilayani Kahama, tulibaini kuta zake kujengwa zikiwa zimepinda

hazijanyooka, pamoja na madirisha ya aluminium kutotosha vizuri," aliongeza. Alisema, katika ujenzi wa kituo cha afya wilayani Kishapu walibaini dosari kwa chemba za majitaka pamoja na milango kujengwa chini ya kiwango na kuagiza kwenye miradi yote hiyo upungufu ulioonekana yafanyiwe marekebisho.

Katika hatua nyingine alisema, ufuatiliaji na usimamizi wa jumuiya za watumiaji maji ngazi ya jamii, walibaini kuwapo na mianya ya rushwa, kuwa jumuiya hizo zinaendeshwa kiholela kutokana na kutokuwapo na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za mapato na matumizi.

Alisema mikakati ya taasisi hiyo katika robo ya mwaka wa fedha (2022/2023), wamejipanga kukamilisha majukumu yao ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ili kuhakikisha inatekelezwa kwa thamani halisi ya fedha iliyotolewa na sio kujengwa chini ya kiwango.

Alitoa wito pia kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, kuendelea kutoa ushirikiano na taarifa za rushwa kwenye taasisi hiyo, ikiwamo ya ujenzi wa miradi kutekelezwa chini ya kiwango ili miradi yote ijengwe kwa ubora unaotakiwa.



Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Shinyanga, Donasian Kessy, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari juzi, kuhusu utekelezaji kwa kipindi cha robo nne ya mwaka wa fedha (2021-2022) kuanzia Aprili hadi Juni. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wanafunzi 200 wasoma darasa moja

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

WANAFUNZI wa shule za msingi Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wanalazimika kusoma katika darasa moja 171 hadi 200 kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa.

Halmashauri hiyo inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 1,097 sawa na asilimia 58 huku vilivyoko ni 972 sawa na asilimia 47.

Pia, inakabiliwa na upungufu wa matundu ya vyoo 3,725 na mwaka huu wa fedha 2022/23, halmashauri imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili kutatua hitaji hilo.

Ofisa Elimu, Vifaa na Takwimu, Mwalimu Prepetua Maige aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili walivyojipanga kutatua upungufu wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo katika shule za msingi na ukamilishaji wa miradi iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Alisema, kuna baadhi ya shule za msingi zina wingi wa wanafunzi na upungufu wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo huku akitoa mfano wa Shule ya Msingi Ilindi yenye wanafunzi 3,757 na vyumba vya madarasa 22 na kusababisha darasa moja kuwa na watoto 171 hadi 200.

Mwalimu Maige alisema, kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha 2022/2023 halmashauri imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi kati ya hiyo Sh. milioni 55 zitatumika kujenga matundu 59 ya vyoo.

Alisema, mpaka sasa wana jumla ya maboma 128 ya vyumba vya madara yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na yanahitaji ukamilishaji ili kuwapatia fursa wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri bila kubanana na kuahidi kuyakamilisha kwa wakati kulingana na bajeti iliyotengwa.

"Shule ya Msingi Bujika vyoo vilititia na wanafunzi wakaanza kutumia vyoo vya shule jirani, wazazi walijitokeza kuchangisha na kuanzisha ujenzi wa matundu ya vyoo 20 nasi tumeshapeleka fedha na vyoo hivyo vimeshakamilika na kuanza kutumika," alisema Mwalimu Maige.

Naye Ester Mathayo, mkazi wa Nyakato alisema, ili kuondokana na upungufu wa vyumba vya madarasa shule za msingi inatakuwa kudahili wanafunzi kulingana na uwapo wa vyumba vya madarasa vilivyoko na sio kudahili wanafunzi ambao watarundikana katika darasa moja.

Kwa upande wake, Magesa William alisema, suala la madarasa na vyoo linatakiwa kupewa kipaumbele katika bajeti za kila mwaka za halmashauri na kuhakikisha miradi yote ya elimu iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi inakamilishwa kwa wakati kwa sababu kuna maboma ya madarasa yana muda mrefu hayajakamilishwa.

# Makarani sensa watakiwa kutunza siri za taarifa

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, John Kayombo, amewaelekeza makarani na wasimamizi wa maudhui wa sensa kutunza siri za taarifa zote watakazozodosa wakati wa zoezi la Sensa ya Watu.

Kayombo ameyasema jana katika mafunzo ya makarani na wasimamizi wa maudhui Tarafa ya Mkongo yanayofanyika, Utete wilayani Rufiji.

Alisema makarani wanatakiwa kuzingatia taarifa zote watakazododosa ni siri na endapo watakiuka utaratibu huo watasababisha serikali kukosa takwimu sahihi.

"Hakikisheni taarifa mtakazo dodosa zinakuwa ni siri hakikisheni mnaelewa vizuri mafunzo haya ili mkatekeleze kwa ufanisi mkubwa kazi hii," alisema Kayombo.

Alitoa msisitizo kwa makarani na wasimamizi hao kutumia vizuri fursa na imani waliyopewa na serikali kuhakikisha sensa inafanikiwa kwa kuwa ndiyo msingi pekee wa maendeleo. Awali, akitoa taarifa ya mafunzo, Mratibu wa Sensa Wilaya ya Rufiji, Faustine Selestine, alisema mafunzo hayo yanafanyika katika vituo Utete chenye makarani na wasimamizi 176 na Ikwiriri, makarani 259. Alisema, mafunzo hayo yamezingatia ushiriki wa watu wenye mahitaji maalumu na kuwa wote wameshafanya majaribio mawili na kufaulu vizuri.

Mafunzo ya Sensa kwa Wilaya ya Rufiji yanafanyika katika tarafa zote tatu na yanatarajiwa kukamilika ifikapo Agosti 18, 2022.




Ukurasa 13

Matunda ya Tunda Man, wenzake yametuozea




KICHEKO CHA SUKARI:

**Kilombero kuongeza kiwanda cha nne cha sukari ni 'K4'**

Ukurasa 14



UCHUMI

# Umeme jotoardhi huu hapa ni megawati 180

• Vyanzo majimoto, kuingia gridi ya taifa 2025

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE



Bomba likitema mvuke unaotoka ardhini 'jotoardhi' ili kuzalisha umeme. **PICHA: MTANDAO**

JOTOARDHI au 'geothermal' ni chanzo cha nishati kinachotumia joto kali lililopo ndani ya miamba ardhini kuzalisha umeme. Kwa sasa habari njema zinaeleza kuwa ifikapo 2025 Tanzania itaanza kufua umeme huo.

Khadija Ahmed, Ofisa Mkuu Mawasiliano wa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi (TGDC), akizungumza na Nipashe, mwishoni mwa wiki anasema, kampuni imetembelea maeneo mbalimbali ikiwamo Mbeya, Songwe na Rukwa kuweka utaratibu wa utafiti na uzalishaji.

Katika mazingira ya kivolkeno ni rahisi kupata vyanzo vya joto ardhi na kutumia mvuke unaotoka au maji moto yaliyopo mita kadhaa chini ardhi kuendesha mapanga boi ya kufua umeme.

Chanzo cha nishati hiyo pia kipo katika Bonde la Ufa la Afrika Mashariki na kwa Afrika Mashariki Kenya tayari, inatumia umeme wa jotoardhi.

Tanzania imo katika mikakakti ya kuzalisha umeme huo, na kwamba ukanda wa nyanda za juu kusini zipo chemichemi za maji moto, ambazo zinafanyiwa utafiti ili kufunga mitambo kufua umeme utakaoongezwa kwenye gridi ya taifa, anasema Khadija.

Kata ya Mkali iliyopo wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa ina kisima kirefu cha maji moto, wakati Ziwa Ngozi mkoani Mbeya pia maji yote ni ya moto aidha, Kijiji cha Nanyara Mbozi mkoani Songwe zipo chemichemi za maji hayo, yote yanaweza kuzalisha umeme, anaongeza.

Anasema wakiwa Mkali wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa kuna kisima kirefu cha maji moto,ambacho kitaanza kufanyiwa utafiti kwa ajili ya kuweka miundombinu au kufunga mitambo ya kuzalisha umeme lengo ni kupata megawati tano.

"Katika Kijiji cha Nanyara wilayani Mbozi mkoani Songwe,utafiti umefanyika na mategemeo ni kupata megawati tano hadi 38 zitakazoingizwa kwenye gridi ya taifa ifikapo 2025 uzalishaji utakapoanza." Anasema Khadija.

Anaongeza kuwa mkoani Mbeya Ziwa Ngozi lenye ukubwa wa zaidi ya kilometa tatu linategemewa kutoa megawati 70 kwa awamu mbili ambazo pia zitaingizwa kwenye gridi ya taifa na ifikapo 2025 wanategemea kuanza uzalishaji.

Busokelo wilayani Rungwe mkoa wa Mbeya,kuna chemichemi za maji moto na utafiti ukikamilika uzalishaji utaanza 2025 lengo ni kupata megawati 60 za gridi ya taifa na kwamba miradi hiyo imefanyiwa tafiti za awali na sasa ni hatua za kuchoronga visima.

Anawataka wananchi kutoa ushirikiano kwa wataalam ili kukamilisha kazi hiyo na kuiwezesha Tanzania inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan inazalisha kwa tija kwenye viwanda na wananchi pia kutokana na umeme kumfikia kila mteja na mwananchi popote alipo.

Mhandisi wa miradi ya moja kwa moja wa TGDC, Cynthia Kulinge, anasema kukamilika kwa miradi hiyo ni fursa nyingine za kiuchumi kwa kuanzisha miradi mingine ya utalii itakayozalisha ajira hasa kwa vijana.

Anasema,katika maeneo husika kutajengwa mabwawa ya kuzalisha umeme na majengo yenye mandhari za kuvutia watalii yatakayotumika pia kukausha mazao,kupasha joto nyumba, kutototolesha vifaranga na kutengeneza bwawa la kuogelea watalii.

Benjamin Otto mkazi wa Kijiji cha Kizombwe, anasema maji moto yanayowazunguka ni chanzo muhimu cha mapato lakini wanakijiji wanaozunguka chanzo hicho, hawanufaiki licha ya kuona wageni mbalimbali wakifika kutembelea na kuiomba serikali kulifanyia kazi suala hilo.

Mkazi wa Rukwa, Peter Sigoma, anasifia maji ya moto akisema yana faida kadhaa, kama wakati wa masika hayajai lakini kiangazi hayapungui wala kukauka na pia yanapikia hata ukiweka muhindi kwa dakika chache unaiva na faida nyingine ni maelezo kuwa kuna uwezekano maji hayo ni chanzo cha mafuta hivyo serikali iangalie uwezekano wa kutafiti na kuyachimba.

**FAIDA JOTOARDHI**

Ofisa wa Mawasiliano Khadija, anasema lina faida lukuki kama kuzalisha umeme likichakatwa linatumika kukuza vimelea vya kuzalisha dawa mbalimbali, huosha bidhaa ngumu, hutumiwa kusindika asali, mafuta ya alizeti na mawese. Pia hutumika kuangua mayai, kufuga samaki na kupasha maji ya kunywa.

Faida nyingine ni kutumika kwa mambo ya sanaa, matibabu ya ngozi, kuchemsha vyakula kama mayai na viazi, burudani kama kuogelea na kujikanda, kupasha vinywaji, kusindika maziwa na kuzalisha umeme.

Ili serikali iweze kutimiza malengo hayo,inatakiwa iongeze jitihada za ziada kulinda vyanzo hivyo kwa kuongeza katazo kwa wakulima,wafugaji na wavuvi ambao wamekuwa wakiharibu mazingira hayo .

UCHUMI

# Kilimo hai tangawizi kinapotua juu ya kaya 550 za wakulima wadogo Same

- Ukulima unalinda watu, mazingira viuatilifu ni asilia
- Mapori hayajaachwa kujazwa miti asilia 11,000

**Na Beatrice Philemon**

TANGAWIZI ni moja ya mazao ya viungo, pia ni tiba kutibu matatizo ya koo, kifua, meno na tumbo. Wakati wa mlipuko wa COVID-19 watu wengi waliona umuhimu wa zao hilo wakiliponda au kulisaga na kutumia pamoja na limao, ndimu, asali kutibu koo na kifua.

Huongeza ladha na harufu ya chai, nyama na pilau pia, inachangamsha vinywaji kuanzia chai, supu, juisi na soda, lakini pia kwenye vilevi na vyakula mbalimbali kama mikate, biskuti, keki, nyama za kusaga na achari inatumika.

Ni malighafi viwanda vya dawa na tiba kama dawa za meno, kifua na kikohozi, tumbo na muwasho wa ngozi pia wanaotengeneza vipodozi kama poda hawajaisahau.

Mikoa inayolima tangawizi ni Kigoma, Tanga, Morogoro, Pwani, Mbeya na Kilimanjaro, hivi karibuni Nipashe inafuatilia kilimo chake mkoani Kilimanjaro ambako Jimbo Katoliki la Same, limejikita kusaidia wakulima wake.

Hadi sasa wakulima 550 kutoka eneo la mardi wamepata mafunzo jinsi ya kulima kilimo hai cha tangawizi na tayari vikundi 18 vya wakulima vimeanzishwa, anasema Meneja Mradi wa Kilimo Hai cha Tangawizi, Jimbo Katoliki la Same, Padri Deogratius Mngumi.

""Jimbo limeona ni bora kuanzisha kilimo hiki ili kulinda afya ya mkulima na mlaji, kuhifadhi mazingira, kuongeza kipato cha mkulima, ubora wa zao na pia kufanikisha juhudi za Tanzania kupata soko la nje," anasema Padri Mngumi.

Anaongeza kuwa Jimbo la Same linawatafutia masoko ya ndani na nje, pia wanakaribisha watu au wakulima kutoka sehemu mbalimbali kujifunza kilimo hicho.

Ni kutokana na faida nyingi za tangawizi na uhitaji jimbo limeona ni muhimu kushirikiana na wakulima ili kulinda afya zao na walaji wanaotumia kiungo hicho ndani na nje ya nchi. Wanafunzwa kulima kwa tija, kulinda afya za wakulima na walaji na kutunza mazingira.

Utafanyika kwa miaka mitatu ukihusisha jimbo na shirika la DKA Austria, ambao ni wafadhili, katika kata za Bwambo, Lugulu na Kirangare wilayani Same, ukinufaisha kaya zaidi ya 540, anasema.

"Unalenga wakulima wote ili mwananchi anufaike na juhudi hizo lazima awe na ardhi, pia mkulima wa tangawizi na mkazi wa eneo la mradi."

Anaeleza kilichowashawishi kuanzisha mradi huu ni kusaidia kupunguza uzalishaji uharibu mazingira na matumizi ya kemikali na viuatilifu (pesticides) kutoka viwandani ambavyo vinaathiri afya za wakulima na walaji.

Meneja Mradi wa Kilimo Hai cha Tangawizi, Jimbo la Same, anasema viuatilifu hivyo wakati mwingine vinasababisha maradhi mbalimbali na kuna madai kuwa watu wanaathirika na magonjwa yanayohusishwa na matumizi ya kemikali za kilimo.

**KILIMO MITI ASILI**

Kupitia mradi huu wakulima wanafundishwa kanuni bora za kilimo ikiwemo upandaji wa miti ya asili ili kulinda mazingira ambapo hadi sasa jumla ya miti 10,000 ya asili imeishapandwa katika maeneo mbalimbali wilayani humo kwenye shule za msingi tano ambazo ni Majengo, Majevu, Njoro na Kirongwe.

Hadi sasa zaidi ya wakulima 550 kutoka eneo la mradi wamepata mafunzo jinsi ya kulima kilimo hai cha tangawizi na tayari vikundi 18 vya wakulima vimeanzishwa kwa ajili ya kilimo hicho.

Anasema kabla ya kuanzisha mradi, jimbo, lilifanya utafiti katika kata hizo tatu na kugundua kuwa wakulima wengi katika kata hizo wanatumia mbolea za viwandani kuzalisha mazao ambazo zimeharibu udongo ambao sasa hauna rutuba, anaongeza .

Pia uzalishaji umepungua kwa sababu ya matumizi ya viuatilifu vya viwandani (pesticides) kiasi kwamba badala ya kupunguza umasikini umeongezeka kwa sababu wakulima wengi hawana kipato cha kununua mbolea na viatilifu, uharibifu wa mazingira unaopunguza mvua na kuongeza ukame umeongezeka na magonjwa ambayo yanasababishwa na viuatilifu yameongezeka pia.

"Ndiyo maana tumeona bora kuja na mradi huu ili kumlinda mkulima, mlaji na mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho," anasema Padri Mngumi.

**MRADI UNAPOLENGA**

Akizungumzia uzalishaji huo Ofisa Ugani, Jimbo Katoliki la Same, Leon Mvungi, anasema katika utekelezaji wa mradi huu wanashirikiana na serikali ya vijiji, kata na halmashauri ya Wilaya ya Same.

"Mradi umelenga maeneo matatu utoaji wa elimu, eneo la kwanza tunafundisha wakulima namna ya kuepuka kutumia dawa za kemikali na mbolea za viwandani, eneo la pili, namna ya kuzalisha mazao mengi na bora pamoja na kupanda miti ya asili na eneo la tatu, jinsi ya kupata masoko bora kwa kuongeza thamani ya mazao hasa tangawizi," anasema

Hadi sasa tangawizi inastawi vizuri katika kata hizo hasa kijiji cha Mamba-Myamba, Bwambo, Vugwama na Kigone.

**VIUATILIFU ASILIA**

Wakulima wamefundishwa jinsi ya kutengeneza mbolea za asili, kuitumia na pia kutumia dawa za asili kuzuia wadudu waharibifu katika mazao, anasema Mvungi.

"Tumewafundisha jinsi ya kutengeneza dawa za asili kwa kutumia alizeti pori, pilipili, mwarobaini na miti mingine ya asili ambayo watu wa zamani waliitumia kuzuia wadudu waharibifu katika mazao," anaongeza Mvungi.

Mbali na hilo wakulima wamefundishwa kanuni za kilimo bora ikiwemo jinsi ya kutayarisha shamba, kuchagua mbegu bora, kupanda kwa wakati na nafasi, kutumia mbolea za mboji na samadi pamoja na kupalilia na kuvuna kwa wakati.



Meneja Mradi wa Kilimo Hai cha Tangawizi, Jimbo la Same, Padri Deogratius (katikati), akikagua kilimo hai cha mboga miongoni mwa wakulima.

> **"Mara ya kwanza niliposikia mradi huu, nilijisikia nafuu sana, niliona kwamba siyo faida ya jimbo peke yake, pia wananchi watanufaika," anasema mkulima huyo mbobezi wa tangawizi.**

Lakini pia wametumia mashamba darasa kutoa mafunzo kwa wakulima ili mkulima aone kwa vitendo zaidi.

Aidha, wamefundishwa kutengeneza mashamba darasa, kutengeneza matuta na walileta mbegu za tangawizi shambani ili mkulima ajifunze kwa vitendo," anasema Mvungi.

Hali kadhalika, anaongeza kuwa kupitia mafunzo haya wakulima wameanzisha kilimo hai cha tangawizi na mazao ya chakula kama vile mahindi, mihogo, magimbi, viazi vitamu na wametunza mazingira kwa kutumia dawa za asili na kupanda miti ya asili kwenye milima.

"Tumetoa mafunzo haya ili watumie kilimo ambacho kinatumia mbolea za asili ambazo ni samadi na mboji na dawa za asili kuzuia wadudu waharibifu wa mazao.

**SAUTI YA WAKULIMA**

Akiongea kwa niaba ya wenzake, mkulima kutoka Kijiji cha Vugwama kata ya Bwambo, Pamelas Mhina, wanashukuru jimbo kuwaletea mradi wa kilimo hai ambacho kitasaidia kujiongezea kipato, kuhifadhi mazingira na kuboresha afya zao.

"Wakati wa mafunzo tulishauriwa tutumie zaidi mboji pamoja na samadi," anasema Mhina akiongeza kuwa hivi sasa, mbolea hizo tunazo kwa wingi, na wataalamu wa kilimo hai wametufundisha jinsi ya kutengeneza samadi pamoja na mboji kwa kutumia mbolea ya ng'ombe na majani yaliyooza kuzalisha mboji ili zitumike kwenye kilimo kuuzia wanaozihitaji."

"Wakulima ambao watahitaji kupata mbolea hizi kutoka kata ya Bwambo, tuna uwezo wa kuzalisha kulingana na mahitji ya mkulima au ekari," anasema Mhina.

Mafunzo waliyopata yamewabadilisha kutoka kwenye kilimo cha kutumia mbolea za viwandani na kuanza kulima kilimo hai ambacho hakitumii mbolea za viwandani, anaongeza mkulima huyo.

"Mara ya kwanza niliposikia mradi huu, nilijisikia nafuu sana, niliona kwamba siyo faida ya jimbo peke yake, pia wananchi watanufaika," anasema mkulima huyo mbobezi wa tangawizi.

Aidha, kutokana na elimu aliyoipata kutoka kwa ofisa ugani na wataalamu wengine wa Jimbo la Same, ametenga robo heka ya kilimo hai cha tangawizi ambayo anatarajia kupata magunia sita. "Fedha nitakazopata nitazitumia kumsomesha mwanangu Chuo Kikuu na nyingine kwa ajili ya shughuli za kilimo," anasema.

**CHANGAMOTO**

"Naamini kilimo hiki kitatusaidia lakini hakuna kazi ambayo haina changamoto, wakulima wengi wameanza kulima zao hili lakini bado wanakodisha mashamba kutoka kwa watu binafsi kwa gharama ya Shilingi 500,000/-kwa mwaka na inategemea unataka kulima kiasi gani au ekari ngapi," anasema Mhina.

Mbali na hilo, wakulima bado wana changamoto ya kupata maji na mabomba ya kuvuta maji kutoka kwenye chanzo cha maji na kupeleka mashambani, bomba hizo zinauzwa kwa gharama kubwa , rola la bomba hizo lenye mita 50 linauzwa 60,000.

Kutokana na tatizo hili, "Tunaomba serikali na Jimbo Katoliki la Same watusaidie kupata mpira kwa sababu mkulima akipata rola ni nafuu ya kutayarisha shamba na atanufaika na zao hili kwa sababu ya umwagiliaji.

**VITENDEAKAZI/ELIMU**

Mhina anasema wanahitaji bomba au rola kwa sababu katika maeneo wanayolima tatizo la maji ni kubwa na yanatoka mbali akisema umbali wa kilomita

INAENDELEA UK.14



Katibu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Same Padri Kasira, akikagua tangawizi kama imewekwa dawa au ni zao la kilimo hai 'pure organic' **PICHA ZOTE: JIMBO LA SAME.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Matunda ya Tunda Man, wenzake yametuozea






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com.

WASWAHILI wana semi mbalimbali zinazotumika kuonyana na kuelimishana.

Mathalan, 'ukicheka na nyani utavuna mabua' na 'mwana mleavyo ndivyo akuavyo'.

Nimekumbuka semi hizi kutokana na tukio la Agosti 8 mwaka huu, siku ya Simba Day, iliyolenga kutambulisha mambo ya msimu mpya wa ligi kuu.

Ni siku ambayo nilipatwa mshituko, niliposhuhudia kitu ambacho sikukitarajia, kikiwa miongoni mwa shamrashamra za klabu hiyo kubwa nchini. Msanii wa kizazi kipya, Khalid Ramadhan 'TundaMan' akifanya kitu cha kushangaza.

Ilikuwa katika ya mechi baina ya Simba na St. Georges ya Ethiopia, wakati wa mapumziko, ghafla wakajitokeza watu wakiongozwa na Msalaba mweupe, wakiwa na jeneza.

Lilikuwa jeneza halisi na si la maigizo kama ambavyo tumezoea kuona, kwani hata Yanga walipata kufanya hivyo, ila tofauti yao lilikuwa jeneza mwanasesere, jeneza la makasha, lisilokuwa na mwili ndani.

Lakini hili la Tunda Man lilikuwa na 'mwili' ndani. Baada ya msafara mpaka kupandishwa jukwaani, lilifunguliwa na 'marehemu' aliyekuwa ndani ghafla 'alifufuka' na mashabiki wa Simba wakashangilia uwanja mzima kuona msanii 'aliyefariki dunia' 'anafufuka!'

Mwongoza sala ya kifo akiwa amevalia mavazi ya viongozi wa dini ya Kikristo, alisoma wasifu wa marehemu huyo, kabla hajafufuka na kukimbia uwanja mzima akiimba nyimbo zake za kuisifia Simba.

Hakika taswira ile haikuwa nzuri si tu kwangu bali hata kwa wengine, tena wakiwamo viongozi wa dini, Wakristo, walioguswa na hatua ile ya kutumia alama za dini kinyume cha maadili.

Hakuna kitu Wakristo wanakiheshimu kama Msalaba, alama muhimu sana ya Mkombozi wao Yesu Kristo, lakini leo unafanyiwa mzaha mbele za watu, huku ukishangiliwa kana kwamba ni jambo jema.

Mbaya zaidi likifanywa na mtoto wa Kiislamu! Sitaki kwenda ndani sana ingawa nasikia kuna hatua zimechukukliwa hapa na pale kuhusu tukio hilo, na bila shaka msamaha pia kuombwa, ila itoshe tu kusema ukicheka na nyani utavuna mabua, kwa nini? Ndio ukweli.

Siku za karibuni, wasanii wamekuwa wakiogopwa, wakipendwa kupitiliza au wakidekezwa kuliko kawaida na wao kujisahau na kudhani hakuna wanachoweza kufanywa hata wakiamua kuchezea alama muhimu za taifa, sembuse Msalaba, Biblia, Msahafu, Rosari au Tasbihi?

Hebu tazama, miaka takriban mitatu iliyopita, nakumbuka pale Kigoma alikuja Rais wa nchi jirani kwa ziara ya kiserikali,

pale uwanja wa Lake Tanganyika, kulifanyika mkusanyiko mkubwa wa kumpokea rasmi mgeni huyo. Msanii aliyekuwa rasmi kumkaribisha, akapandishwa jukwaani na kumwimbia Rais wa nchi akiwa na mwenyeji wake, wimbo wa 'Uno', wimbo unaosifia kiuno cha mwanamke kana kwamba hatuna nyimbo za kitaifa! Lakini aliimbiwa Rais huyo akiwa na mwenyeji wake na kulazimika kushangilia.

Ni msanii ambaye kuna wakati katika sherehe za kitaifa alimwimbia Rais aliyekuwapo enzi hizo, akimsifia na hatimaye Rais huyo akamtaka msanii huyo akagombee ubunge kwao. Fikiria alijisikiaje msanii huyo, kuombwa na mkuu wa nchi akagombee ubunge!

Kama hiyo haitoshi, katika sherehe nyingine katika uwanja wa Mkapa, msanii mwingine mbele ya marais wageni waliohudhuria, akadiriki kutamka kuwa majeshi yetu yamelala sana, sasa inafaa

tukayajaribu dhidi ya nchi jirani! Rais wa nchi hiyo jirani na mwenyeji wake wakimsikiliza na kulazimika nao kupiga

makofi. Mwingine ambaye si msanii halisi, naye hivi karibuni, akiwa amefungiwa kujihusisha na jambo fulani, kwa muda

fulani, naye akaona isiwe tabu katika Siku ya Mwananchi, akaamua kuingia uwanjani na kufanya alichokatazwa, kwa mshangao wa baadhi ya watu, lakini kwa furaha ya wengine.

Mambo yote haya yanafanyika bila wasimamizi kufuatilia ratiba ya nini kitafanyika wapi, saa ngapi na kwa namna gani! Kama hayo hayafanyiki, utendaji bora uko wapi?

Kuna siku tutaendelea kuyaendekeza haya, ndipo msanii kwa deko, ataingia uwanjani na mabomu na kuyalipua na matokeo yake tutabaki tunaugulia na kulia huku tukisaga meno kama mbwa.

Haya ndiyo matunda ya kina Tunda Man na wenzake. Tukidharau miiba hii tutaota matende huku tukicheka walahi! Alamsiki!

BIASHARA

# Kilombero kuongeza kiwanda cha nne cha sukari ni 'K4'

• Ahadi kwa wakulima wa nje 'miwa yao haitaharibika'

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAKULIMA wa miwa wanaweza kupata tija kwa kuvuna tani nyingi, kuuza na kuendelea kufurahia maisha ya kipato kikubwa iwapo watapanda vipande vya miwa kwa kuvilaza badala ya kuotesha jicho moja.

Meneja wa mafunzo ya vipando(mbegu) wa kiwanda cha sukari Kilombero mkoani Morogoro, Tumaini Sawe, anasema kwenye banda la kilimo la Bodi ya Sukari Tanzania, wakati wa Maonyesho ya Nane Nane Kanda ya Mashariki yanayofanyika Uwanja Mwalimu Julius Nyerere.

Sawe anawashauri wakulima kutumia mbinu za kisasa za kuotesha miwa kwa kuilaza na kuachana na kupanda 'jicho' akisema ni mbinu ya kizamani.

Anasema kulaza kipande cha muwa kuna nafasi kubwa ya kutumiwa na wakulima wadogo na wa kati kwa sababu haihitaji gharama kubwa kama kuotesha jicho mbinu inayotumika na baadhi ya viwanda.

Mbinu hiyo humlazimisha mkulima ama kiwanda kuotesha jicho moja kulihudumia ili baadaye linapostawi kulipanda shambani jambo linalochosha.

Sawe anawaambia, wakulima wengi wamekuwa wakitumia kilimo cha kizamani cha kuchomeka miwa, lakini baadaye hakuna tija sababu hauongezi vipando wala miwa shambani ili kukuza uzalishaji na kwamba wakitumia mbinu za kisasa za kupanda miwa kwa kulaza watanufaika kwa kupata vipando vingi huku wakiotesha jicho wataweza zaidi.

Mratibu wa kitaifa kutoka kituo cha utafiti wa mbegu- TARI Kibaha, Minza Masunga, anawashauri wakulima wa miwa kutumia aina nne mpya za mbegu zilizotafitiwa ili kukabiliana na changamoto ya wadudu na udumavu.




Meneja mafunzo ya mbegu wa kiwanda Sukari Kilombero, Tumaini Sawe, akielekeza wakulima kupanda kisasa na siyo kuchomeka mbegu ardhini. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

Masunga anazitaja aina hizo mpya zilizopitishwa kuwa ni pamoja na N 47, R 570, TARISCA 1 na 2, akisema wakulima wa miwa wamekuwa wakitumia mbegu za muda mrefu ikiwamo NCO 376 ambazo hazina faida.

Anasema mbegu hiyo inashambuliwa na wadudu na kuleta udumavu wa mazao shambani na kwamba imeshusha kwa asilimia 50 hadi 70 sukari kwenye muwa.

Aidha, anasema matumizi ya mbegu mpya yanafanikisha kuleta ukinzani kwa wadudu mbalimbali kama 'fungwe' wanaoshambulia miwa na kupunguza sukari kwenye muwa kwa asilimia kubwa.

Mkufunzi mwandamizi kutoka Chuo cha Sukari cha Taifa (NSI) Mwanaidi Jafary, anawataka vijana waliomaliza kidato cha nne kujiunga na mafunzo ya uzalishaji miwa ili kufanikisha juhudi za serikali za kupata wataalamu zaidi na kuongeza uzalishaji wa sukari na kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

**UZALISHAJI KUONGEZEKA**

Ofisa kilimo wa wakulima wa nje kutoka kiwanda cha sukari Kilombero Barka Salim, anawataka wakulima wa miwa nchini na wengine kujikita kwenye kilimo cha miwa ili kukidhi mahitaji ya kampuni ya Sukari Kilombero inayopanua uzalishaji na kufungua kiwanda kipya cha K-4 ifikapo 2024.

Anasema kiwanda hicho kinatarajia kuchakata zaidi ya tani milioni 1.5 za miwa kutoka tani 600,066 za sasa na katika upanuzi huo serikali itatoa asilimia 25 na kiwanda ambacho ni wawekezaji asilimia 75.

"Wakati umefika wakulima kuanza kupanua mashamba na kuanzisha mapya ili kutumia fursa hiyo ya kiwanda kukuza uchumi wao na wa taifa lakini pia kufanikisha juhudi za kuzalisha sukari na kutosheleza mahitaji nchini."

Salim anasema awali wakiwa na viwanda vya K-1 na K-2 walikuwa wanachakata tani 600,000 hadi 666,000 za miwa kwa msimu uliopita kutoka hekta zaidi ya 15,000 za wakulima wa nje na 11,000 za kampuni ikiwa ni jumla ya hekta 26,000.

Anasema kiwanda hicho kipya mbali na kusaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kupata mauzo mengi pia kitaondoa kero mbalimbali ikiwa ni kuongeza nishati kwa vile mabaki ya miwa hutumika kuzalisha umeme kuzuia yasitoke nje na kusumbua jamii.

Aidha, anafafanua kuwa wakulima wa kilombero wanazalisha miwa zaidi ya tani 600,000 zinazopokelewa na kiwanda lakini miwa mingine inabaki shambani hivyo, Kilombero ikaamua kuanzisha kiwanda cha nne ili kukabiliana na tatizo la miwa iliyokuwa inaharibika na kupokea mingine kutoka kwa wakulima.

"Miwa ya sukari ina saa chache kutoka kuchomwa hadi kutengenezwa sukari, sasa hivi saa nyingi zinaongezeka kutokana na uwezo wa kiwanda na wingi wa miwa, tunachakata miezi tisa lakini kiwanda kipya kikikamilika tutufanyakazi hiyo kwa miezi saba na kumaliza miwa. Kitaalamu inapaswa kuanzia kuchoma hadi kutengeneza sukari zisizidi saa 60 lakini kimkataba wao ni saa 120 sababu ya uwingi wa miwa na viwanda vinashindwa kumudu. Tunategemea K-4 itamaliza tatizo hilo" anasema Salim.

Wakulima wa miwa Mtibwa wilayani Mvomero mkoani hapa wanaiomba serikali kuangalia uwezekano wa kutoa bei elekezi ya ya miwa viwandani ili wanufaike na kilimo hicho kama wanavyonufaika wakulima wa Kilombero.

Ally Mayogo anasema ni wakulima wa miwa wa muda mrefu ambao wanauza miwa kiwandani Mtibwa kwa bei ya Sh 70,000 kwa tani tofauti na Kilombero ambako wananunua tani kwa 120,000.

Mkulima mdogo wa miwa kutoka Kilombero, Bakari Mkangamo anawataka wakulima kujikita kwenye kilimo cha miwa kwa sababu kimemtoa kwenye hatua moja kwenda nyingine na sasa ana nyumba mbili anasomesha na ana kipato kizuri.

Mkulima wa miwa Mkulazi Kasubi, anawashauri wakulima wengine kulima miwa kwani kilimo hicho kina tija na kinaleta maendeleo kwao na taifa kwa haraka

Kasubi Mwenyekiti wa chama cha ushirika wa miwa Magole anawashauri wakulima wakitaka kutajirika akieleza kuwa heka moja kuanzia kupanda hadi kuvuna inagharimu Shilingi milioni 1.2 hadi 1.6 na faida ni milioni 2.5 inayopatikana baada ya siku 45.

Anasema kwa kawaida mkulima huuza tani moja ya miwa Shilingi 120,000 na wakulima wengi huvuna kuanzia tani 40 hadi 80 na wao wamejiwekea lengo la chini kuwa ni kupata tani 45 na kwamba mkulima akimaliza taratibu zote za kukata, kusomba, kupakia hadi kufikisha kiwandani atafahamu amepata kiasi gani cha fedha kwa sababu kilimo hicho pia hakina wizi.

INATOKA UK.12

## Kilimo hai tangawizi kinapotua juu ya kaya 550 za wakulima wadogo Same

14 hadi kufika mashambani.

Ili kupata maji kwa ajili ya kilimo hiki, hivi sasa wakulima wanavuta maji kutoka kwenye makorongo na mto Safeni unaotokea kwenye msitu wa Shengena ambao unaleta maji mpaka Kihurio, mto huu unatiririsha maji kata za Bwambo Ndungu.

"Tunaomba serikali itusaidie kujenga miundo mbinu ya maji au kuvuta maji kutoka sehemu zenye maji kuleta mashambani ili mkulima aweze kunufaika na kilimo hiki. Mbali na hilo, wakulima wanahitaji kupewa nguvu kidogo hasa upatikanaji wa mbegu za tangawizi.

"Ukiangalia wakulima wengi wanaolima zao la Tangawizi hawana mashamba wanatumia fedha nyingi kukodisha mashamba na pia wana changamoto ya upatikanaji wa mbegu,"anasema.

"Tunahitaji mafunzo kuhusu kilimo hai kwa sababu elimu tuliyonayo siyo ile ya darasani ni ya mchapakazi, wakulima wakipewa mafunzo jinsi ya kuchanganya mbolea pamoja na kutumia madawa ya asili waliofundishwa hapo awali watalima kwa ufanisi zaidi kwa sababu watakuwa na elimu ya kutosha." Anasema.

Wanahitaji mafunzo jinsi ya kuhifadhi mazao kwa kutumia dawa za asili baada ya kuvuna ili yasibunguliwe na wadudu.



# Waomba fidia kupisha mradi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa eneo la Njedengwa West, jijini Dodoma wameiomba serikali kuwasaidia kulipwa fidia ili kupisha mradi wa upanuzi wa barabara.

Takriban nyumba 97 zitarajiwa kuvunjwa ili kupisha upanuzi huo wa barabara mradi unaotekelezwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Mmoja wa wakazi hao, Emmanuel Makasi, akizungumza juzi kwenye mkutano na waandishi wa habari katika eneo hilo, alisema wameishi hapo kwa muda mrefu lakini wanashangaa hivi karibu TARURA wanataka kuvunja nyumba zao bila kuwalipa fidia.

Alisema hivi karibuni walikuja watumishi kutoka TARURA na kuanza kuweka alama za kuvunja nyumba zao (kuweka alama X) hali ambayo inawapa shaka juu ya hatima yao na makazi yao.

"Tupo hapa kwa ajili ya kuomba kupata mustakabali wa haki yetu kwani awali alikuja mkuu wa wilaya mheshimiwa Jabir Shekimweri, tukamweleza tunachotaka akasema anakwenda kujadiliana na wenzake halafu atakuja kutupa majibu.

"Tulikubaliana hakuna shughuli yoyote itaendelea hadi kupata suluhu lakini hadi leo (juzi) hii hajarudi kutupatia majibu yoyote na tunashangaa kuona ambavyo leo wanakuja watu bila taarifa na kuanza kuweka alama za kuvunja makazi yetu bila kutueleza nini hatima yetu," alisema Makasi.

Alisema wanamwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati mgogoro huo ili wapatiwe haki yao ya msingi ambayo iko hatarini kupotea.

"Tunamwomba Rais wetu atusaidie kupata haki yetu kwani nyumba zetu zipo hatarini kubomolewa tunaomba kama wanataka kutuondoa basi watulipe ili twende kutafuta makazi eneo jingine, kwani ni ajabu hivi sasa wanalipa makaburi harafu sisi wenye nyumba wanataka kutuomba hivihivi," alisema.

Nenelwa Jeremia, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema viongozi wa Jiji la Dodoma wanapaswa kubadilika kwa kuwa kila mara eneo hilo ndilo limekuwa likikumbwa na kero za bomoabomoa.

"Kwa nini kila siku Njedengwa ndiyo watu wa kuwaonea? Tumewakimbia kule lakini bado pia hapa tumefuatwa kuwa tumejenga barabarani. Rais pamoja na Waziri Mkuu wamekuwa wakisema mradi ukimkuta mtu katika eneo lazima alipwe fidia. Sasa tunaomba haki itendeke kwetu pia tuna watoto wadogo na wengine ni wajane kwani sisi si Watanzania?" Alihoji

Mkuu wa Wilaya Dodoma, Jabir Shekimweri, alipoulizwa na Nipashe kuhusu hilo, alikiri kufahamu malalamiko hayo na tayari alishakutana na wananchi hao.

"Haya malalamiko niliyafahamu wakati ambapo nilikwenda kufanya ziara ya tathmini ya mradi huu wa upanuzi wa barabara lakini nilikutana na hoja nyingine. Wengine walidai kuwa wananchi awali walikubali kupisha bila fidia, wengine walipatiwa maeneo mbadala lakini yalishavamiwa na wengine walidai ni wazee hivyo kuwahamisha pale isingekuwa jambo la busara.

"Lakini niwaahidi kwenda kuona ni jinsi gani tunapata njia ambayo kila mtu ataridhika. Nilipanga kwenda lakini kuna mambo kidogo yalibana kwenye ratiba lakini wikiendi hii au wiki ijayo nitakwenda kukutana nao na kupata suluhu ya malalamiko yao," alisema Shekimweri.

# Hatima katibu mkuu Anglikana Agosti 26

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HATIMA ya mgogoro wa Kanisa la Anglikana Tanzania na aliyekuwa katibu mkuu wake, Dk. Mecka Ogunde, inatarajiwa kujulikana Agosti 26, mwaka huu, ambapo Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) itatoa uamuzi mdogo baada ya jana kusikiliza maelezo ya pande zote.

Hatua hiyo ni baada ya kusikiliza majibu ya upande wa mlalamikaji kuhusu mapingamizi yaliyowasilishwa na upande wa mlalamikiwa.

Juzi, upande wa mlalamikaji uliwasilisha majibu kupitia wakili wake, Willson Ogunde, mbele ya Msuluhishi Mfawidhi Mkoa wa Dodoma, Rodney Matalis.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kujibu mapingamizi hayo, Wakili Ogunde alidai kuwa wamejibu hoja mbili zilizowasilishwa na upande wa mlalamikiwa.

"Kabla ya kuanza kesi ya msingi, kama kuna mapingamizi lazima yajibiwe kwanza, hivyo leo (jana) tulipatiwa nafasi ya kujibu mapingamizi yaliyotolewa na upande wa pili ambao walikuwa na hoja nne lakini wao wenyewe walizipunguza na kubaki mbili ambazo wanadai kuwa tume haina mamlaka ya kusikiliza shauri hili kwa kuwa limekaa kidini zaidi.

"Hoja ya pili wanadai kuwa mteja wetu hakufuata katiba katika kuja kufungua shauri hili. Tumefanikiwa kuwajibu hoja zote na tumepangiwa Agosti 26, mwaka huu, uamuzi mdogo utatolewa na msuluhishi kama mapingamizi hayo yamekubaliwa au yamekatiliwa ili kesi ya msingi ianze kusikilizwa," alidai Ogunde.

Wakili wa mlalamikiwa, Sosthenes Mselingwa, alidai kuwa pande zote mbili zimetoa maelezo yao na wanasubiri uamuzi utakaotolewa Agosti 26.

"Kimsingi mapingamizi yetu ilikuwa tume hii kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri hili kwani lilifaa kutatuliwa na Kanisa Anglikana Tanzania. Lakini pia mlalamikaji alipaswa baada ya kuondolewa na nyumba ya maaskofu, alipaswa kwenda kwenye Baraza la Rufani," aliongeza.

Julai 27, mwaka huu, Wakili Ogunde alidai kuwa wamefikia uamuzi hayo baada ya Baraza la Wadhamini la Kanisa Anglikana Tanzania, kushindwa kufika makubaliano na mteja wake.

Hata hivyo, upande wa mlalamikiwa uliwasilisha hati kinzani, mapingamizi ambayo waliomba muda kwenda kuyapitia ili kutolea majibu.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma juzi, wakati alipofika, kujitambulisha baada ya kuhamishiwa mkoani humo akitokea Mkoa wa Geita. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CCM yakusanya mil. 178/- ubunge Afrika Mashariki

**Augusta Njoji (DODOMA) na Magdalena Jackson (SJMC)**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimevuna Sh. milioni 178 kwa makada waliojitokeza kuchukua fomu za kuomba kuwania ubunge wa Afrika Mashariki.

Fomu hizo zilikuwa zikitolewa kwa gharama ya Sh. milioni kila moja na hadi juzi kufungwa kwa pazia la uchukuaji fomu, makada 178 walikuwa wamechukua na kurejesha fomu.

Hata hivyo, makada hao kwa sasa wanasubiri wachujwe kwenye vikao mbalimbali kwa mujibu wa taratibu za CCM.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Organaizesheni, Dk. Moudline Castico, aliwataka wagombea hao kuwa watulivu na subira na waendelee na shughuli zao hadi pale taarifa nyingine itakapotolewa.

"Kwa idadi hii ya wagombea wa ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) waliojitokeza kuchukua na kurejesha fomu, ni ishara tosha kwamba CCM ndicho chama pekee kinachojali na kuzingatia haki na wajibu wa wanachama wake katika dhima ya demokrasia," alisema.

Aliwataja waliojitokeza kuwa ni pamoja Dk. Ally Nkwabi, Zabron Wakalo, Ezekiel Maige, Clion Dismas, Leonard Masai, Edna Chandeu, Josephelias Sabuka, Martin Lissu, Fadhili Maganya, Frank Machui, Wemael Chamshama, Mshinwa Banzi, Mshindi Lyamuhulu, Dk. Leonard Subi, Emelda Mwamanga, Lusubilo Mwakabibi, Jalia Mayanja, Ussy Charugamba, Ally Mandai, Zena Simkondo, Edward Nyerere, Gwakisa Makaranga, Gidion Mandesi na Janice Kimaro.

Wengine ni Doto Nanauka, Sahila Wilfred, Evangel Otieno, Malema Eli, Loman Mollel, Joel Nanauka, John Haule, Lameck Jaston, Mwamvua Sykes, Bashira Nabhaniy, Diana Obare, Arafa Mashi, Baltazar Awe, Frank Mbele, Fredy Katembo na Yussuf Suleiman Khalfan.

Pia yumo Suzana Kabula, Itikija Mwanga, Neema Mwinge, Getrude Haule, Lwitiko Anyingisye, Salum Kanyungu, Edna Mafuwe, Dk. Salvatory Mhando, Godfrey Simbeye, Elias Komba, Consolata Mulalo, Lunus Linda, Lathifa Skyes, Dk Hamad Juma, Fatma Omar.

Wengine waliojitokeza ni Devotha Mbonamasabo, Daniel Okoka, Johnson Mgimba, Benedict Kikove, Asteria Mathias, Abdalla Masauri, Dorice Mgetta, Laurence Ngolly, Mona Mangula, Faraja Malaki, Nafue Nyage, Francis Songoro, James Millya, Theddy Patrick, Mhandisi Caroline Lyimo, Hamis Rajabu, Daudi Majinge, Methusela Mbajo, Crescentius Magori, Benedict Kikove, Mhandisi Frank Mejooli, Aloyce Mushi.

Aliwataja pia Comfort Maugo, Mussa Mgata, Doris Mollel, Julieth Rushuli, Alfred Elia, Alfred Sallwa, Gilbert Bankobeza, Doreen Noni, Deodatus Kinawiro, Shedrack Mashauri, Israel Ilunde, Machano Ali Machano, Rahma M. Ibrahim, Sabra Zubeir Said na Faki Ame Kesi.

Castico alisema pia wamo Nasikiwa Berya, Amina Mgeni, Ambwene Kajula, Nasser Nzamba, Prackseda Marmo, Maria Kangoye, Shogo Mlozi, Godfrey Shirima, DK Paul Anthony, Henry Bulengera, James Kasurura, Alfa Munyi, Manase Michael, Ayubu Lemilya, Nicksoni Kahimba na Mhandisi Haji Vuai Ussi.

Wanachama wengine ni Brigedia Jenerali Mstaafu Marianus Mhagama, Mwanamanga Mwanduga, Conrad Lushakuzi, Balozi Anastase Rwegayura, Khadija Kayanda, Elibahati Lowassa, Masengwa Busigosolwe, Thomas Kitima, Reginald Shirima, Luvuva Salum Ali, Dk. Abdallah Hasnuu Makame na Mmanga Mjengo Mjawiri.

Pia wamo Jonas Lufungulo, Dk Linda Salekwa, Loti Lembrice, Richard Mbuguni, Angela Kiza, Wakili Msomi Pascal Mayala, Francis Nanai, Melinda Muganda, Fikiri Luganga, Mkondo Fabian, Albert Mbago, Robison Etuttu na David Mwakanjuki, Amani Kajuna, Azizi Mussa, Judith Mollel, Amedeus Mzee, Kalunde Malale na William Reuben, Fancy Khuni, Salma Mwassa, Ngwaru Maghembe, Happyness Lugiko, Shabu Makonyola na Salimu Kungulilo.

Wengine ni Norman Sigalla, Harrison Lukosi, Rehema Hassan, Ahmed Nkhuli, Steven Mkomwa, Dorica Gwilenza na Ansar Kachabwa, Nadra Juma Mohamed, Ahmed Shehe Saleh, Maryam Said Mussa na Mourice Oscar Sendera.





## Wafurahia kutatuliwa kero kwa kujengewa mradi wa maji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Mji wa Makongolosi katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya wameishukuru serikali kwa kuwatatulia kero ya maji kwa kuwajengea mradi mkubwa wa maji ambao umemaliza kabisa tatizo la maji katika kata hiyo.

Serikali imejenga mradi wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.8 kwa ajili ya kuhudumia kata mbili za Mji huo ambazo ni Kata ya Makongolosi na Kata ya Bwawani ambazo kabla zilikuwa zinategemea maji ya visima na kwenye mito.

Mmoja wa wananchi hao, Lawena Nsonda, mmiliki wa Shule ya Hollyland alisema wawekezaji wengi walikuwa wanashindwa kuwekeza kwenye maeneo hayo kutokana na tatizo la maji.

Alisema wawekezaji hao walikuwa wanalazimika kuchimba visima lakini kwa sasa gharama hizo wataondokana nazo na badala yake watakuwa wanavuta maji hayo ya bomba.

"Hapa sasa hivi tunaogelea tu maji, tunamshukuru Rais wetu kwa kutusaidia mradi huu maana kwa miaka mingi tulikuwa tunapata shida kubwa ya maji," alisema Nsonda.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi alifanya ziara katika mradi huo hivi karibuni na kuagiza ukamilike haraka ili wananchi waanze kupata huduma.

Alisema serikali iliamua kutumia fedha nyingi kutekeleza mradi huo ili kuwasaidia wananchi hao.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (katikati), akionyesha kadi maalumu ya machinga kutoka Benki ya NMB, kwa machinga alipotembelea soko la Old Airport la jijini Mbeya mapema wiki hii. Kulia ni Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola na Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wajengewa ghala la kisasa kuhifadhi vitunguu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SOKO la vitunguu vinavyozalishwa katika Skimu ya Umwagiliaji ya Igomelo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, imeanza kuimarika baada ya wakulima hao kujengewa ghala la kisasa lenye uwezo wa kuhifadhi mazao hayo kwa muda mrefu bila kuharibika.

Aidha, upotevu wa mazao ya wakulima baada ya mavuno unatajwa kuwa umepungua kwa zaidi ya asilimia 85 ikilinganishwa na ilivyokuwa awali walikuwa wanapoteza mazao mengi baada ya mavuno.

Wakulima hao wamejengewa ghala hilo na Shirika la HELVETAS kupitia mradi wa KIBOWAVI, ambao ni sehemu ya Utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Mnyororo wa Thamani wa Kahawa, chai na mazao ya bustani ijulikanayo AGRI-CONNECT.

Juzi maofisa kutoka wizara za kisekta zinazotekeleza miradi ya AGRI-CONNECT pamoja na mashirika yanayotekeleza miradi hiyo walifanya ziara katika eneo hilo kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa mradi huo na wakulima walisema wameshaanza kunufaika.

Mmoja wa wakulima hao, Julius Kumwenda, alisema kabla ya kujengewa ghala hilo walikuwa wanapoteza mazao mengi kutokana na vitunguu kuoza vikiwa vimehifadhiwa.

Alisema kutokana na hali hiyo walikuwa wanalazimika kuuza mazao yao baada ya kuvuna wakihofia wakihifadhi yataoza na kuingia hasara zaidi ya ile ambayo wanaipata kwa kuuza kwa bei ya chini.

Alisema maghala waliyokuwa wanayatumia yalikuwa ya kienyeji na kupoteza zaidi ya nusu ya mavuno yao na kushindwa kuendelea na kilimo.

"Niliwahi kutunza magunia 300, lakini ambayo yalipona kuharibika yalikuwa 30 pekee, lakini kwenye hili ghala jipya ambalo tumejengewa nilihifadhi magunia 300 yaliyoharibika ni mawili pekee na vitunguu hivi vinakaa zaidi hata ya miezi sita," alisema Kumwenda.

Naye Daud Chengula, alisema kutokana na ubora wa ghala hilo wana uwezo wa kutunza mazao yao wakisubiri bei ipande tofauti na ilivyokuwa mwanzo na walikuwa wanauza mazao yao kwa bei ya chini.

Alisema kutokana na hali hiyo wakulima walikuwa wanapata faida kidogo au kutopata kutokana na mazao yao kuuzwa kwa bei ya chini.

Mwenyekiti wa Skimu ya Igomelo, Nelson Peter, alisema pamoja na uwapo wa ghala hilo, bado wanakabiliwa na tatizo la vipimo vya kinyonyaji ambavyo wanunuzi wanavitumia wakati wa kununua mazao hayo.

Alisema wanunuzi wengi wananunua kwa kutumia kipimo chenye ujazo mkubwa maarufu lumbesa ambacho alisema kinawanyonya.

Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji wa miradi kutoka Shirika la HELVETAS, Shoma Nangale, alisema walijenga ghala hilo kwa kushirikiana na halmashauri ya Wilaya ya Mbarali pamoja na Chama cha Wakulima cha Igomelo (AMCOS).

Alisema, pia wanawasaidia wakulima kuwaunganisha na masoko ya uhakika kwa ajili ya kuuza mazao yao na kuwaunganisha na fursa zaingine muhimu.

"Tunawawezesha pia wakulima kuzijua fursa zingine ambazo zipo kwenye kilimo, kwa AMCOS hii ya Igomelo tumewasaidia kwenye miundombinu na elimu," alisema Shoma.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Kilimo, Ngugo Mibavu, aliwashauri wakulima wa skimu hiyo kuyatumia mapato wanayoyapata kwenye kilimo hicho kujenga maghala mengine ili kujiimarisha zaidi kimapato.

Alilipongeza Shirika la HELVETAS kwa kujenga ghala hilo kwa maelezo kuwa linaendana na thamani ya fedha zilizowekezwa kwenye mradi huo huku akiwataka waendelee kutekeleza miradi mingine.

# Kukamilika mradi kwakomboa wananchi Mbeya

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

WAKAZI wa vijiji sita vya kata za Mshewe na Mjele katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameondokana na tatizo la kutembea umbali mrefu kufuata maji baada ya serikali kukamilisha mradi wa maji wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.3.

Aidha, wananchi hao wanaeleza kuwa pamoja na kwamba walikuwa wanafuata huduma hiyo umbali mrefu lakini maji waliyokuwa wanatumia usalama wake ni mdogo kutokana na kuchangia na mifugo pamoja na wanyama wa porini.

Wananchi hao waliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ambaye aliongozana na maofisa wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kwa lengo la kukagua mradi mbalimbali.

Mmoja wa wananchi hao, Faines Kapange, alisema walikuwa wanalazimika kuamka usiku kwenda kufuata maji mto Mbalizi hali ambayo ilikuwa inahatarisha usalama wao.

Alisema tatizo hilo lilikuwa linasababisha migogoro kwenye ndoa kutokana na kutumia muda mrefu kwenda kufuata huduma hiyo na wakati mwingine kushindwa kufanya shughuli zingine za maendeleo.

"Tunapoona maji yanatoka kwenye bomba hatuamini, mimi nimezaliwa hapa Mjere na nimekulia hapahapa sijawahi kuona maji ya bomba, tunaishukuru sana serikali kwa kutuletea huduma hii," alisema Faines.

Naye Felister Saul alisema, walikuwa kwa wale ambao walikuwa hawana uwezo wa kufuata maji mtoni walikuwa wanalazimika kununua Sh. 500 kwa ndoo moja ya lita 20.

Alisema walikuwa na maisha magumu ambayo yalikuwa yanawafanya wasiipende serikali yao, lakini baada ya mradi huo kukamilika na kuanza kunufaika wameanza kuiamini.

Kaimu Meneja wa RUWASA wa Wilaya ya Mbeya, Mhandisi Tupeligwe Msojo, alisema mradi huo utawanufaisha wananchi zaidi ya 11,000 wa vijiji hivyo ambavyo vinalengwa kunufaika na mradi huo.

Alivitaja vijiji vitakavyonufaika na mradi huo kuwa ni Mshewe, Mumvwa na Mapogoro ambavyo vipo kwenye Kata ya Mshewe pamoja na Mjele, Chang'ombe na Njelenje ambavyo vyote vipo katika Kata ya Mjere. "Mradi huu unaendelea na sasa hivi tunachokifanya ni kujenga matangi ya kuhifadhia maji kwenye maeneo matano na tunajenga vituo 36 vya kuchotea maji na katika kijiji hiki cha Mjele wananchi wameanza kunufaika," alisema Tupeligwe.

Alisema pamoja na umuhimu wa mradi huo kuwa na umuhimu kwa wananchi, kuna baadhi yao wanahujumu miundombinu kwa kuiba mabomba, kuchoma mkaa juu ya mabomba na kuyapasua pamoja na kung'oa mawe ya alama za bomba.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Njeza aliwataka wananchi hao kuitunza miundombinu ya maji hayo ili idumu na kuwasaidia kwa muda mrefu zaidi.

Njeza alisema kuwa pamoja na kwamba miradi inatekelezwa na serikali, lakini miradi hiyo ni ya kwao wenyewe na kuwataka kuhakikisha wanaitunza kwa hali na mali pamoja na kuhakikisha wanachangia huduma hiyo.

Alisema baada ya kukamilika serikali itawakabidhi kwa ajili ya wao wenyewe kuendelea kuiendesha kwa kununua baadhi ya vifaa vitakavyokuwa vinaharibika.





# Waziri asema mabadiliko ni lazima sekta ya habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita, amesema sekta ya habari kwa sasa inahitaji sera inayokwenda na wakati ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia duniani na yanayolinda maslahi ya wanahabari.

Aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Kariakoo Mjini Zanzibar wakati akifungua mkutano wa kitaifa kuhusu mageuzi ya sekta ya habari Tanzania ambao umeandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kupitia mradi wa kuwainua wanawake na vijana.

Waziri Tabia alisema bado mazingira ya wanahabari hayaridhishi na sekta ya habari inakabiliwa na idadi ndogo ya wanahabari wanawake, mishahara finyu, wengi hawana mikataba ya ajira na kuna tatizo la rushwa ya ngono.

Alisema lazima kuwapo kwa mifumo inayowezesha wanahabari kufanya kazi kwa usalama na wamiliki wa vyombo vya habari kufuata sheria ili kulinda maslahi ya wanahabari nchini.

Suala la ukatili wa kijinsia katika vyombo vya habari, alisema limekuwa likilalamikiwa na wanahabari wengi hali ambayo imesababisha kuwapo kwa idadi ndogo ya wanawake wanahabari katika tasnia hiyo.

Waziri huyo alisema ukatili wa kijinsia ndicho chanzo cha wanahabari kushindwa kutimiza majukumu yao ikiwamo uandishi wa habari zinazolenga usawa wa kijinsia, hivyo kuwapo mifumo rasmi inayolinda usalama wa wanahabari kutasaidia kutokomeza kwa vitendo ukatili wa kijinsia.

Alisema Zanzibar iko katika mchakato wa rasimu ya Sera ya Utangazaji Zanzibar ya mwaka 2008 ambayo inabadilishwa na hivi sasa Sheria ya Habari Zanzibar iko katika mchakato wa marekebisho ambao umefikia ngazi ya makatibu wakuu na hatimaye ipite serikalini ili kuendana na hali halisi ya wakati uliopo.

Kwa mujibu wa waziri huyo, serikali ya Zanzibar imejipambanua katika kuboresha maslahi ya wanahabari na wameitengeneza kada ya habari kuwa kada maalum na imeshakamilisha muundo wa habari ili kuwa na takwimu za wanahabari na kuthamini mchango wao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alisema usalama wa waandishi wa habari ni muhimu wanapokuwa kazini ili kufanya kazi katika mazingira ambayo hakuna rushwa ya ngono na kupata maslahi yao ya kiusalama na kifedha.

Katibu wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdallah Salum, alisema mjadala huo utahusisha masuala ya jinsia katika vyombo vya habari na mjadala huo utatoa maazimio katika kuhakikisha maslahi ya wanahabari, usalama wao na jinsia katika vyombo vya habari vinapewa nafasi.

"Vyombo vingi vya habari wasimamizi ni wanaume lakini mwelekeo sasa ni kuwapa nafasi wanawake ili kufaidi ulezi wa wanawake katika vyombo vya habari na tasnia yetu ya habari kupata nguvu na kuondokana na mfumo dume katika vyombo vya habari," alisema Katibu huyo.

Naye Meneja Program wa Shirika la Kusaidia Waandishi wa Habari Kimataifa (IMS) Feusta Msoka, alisema waandishi wa habari wanapata vitisho mbalimbali kutokana na habari wanazoandika hasa wanapoandika habari za ukatili wa kijinsia.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, akizungumza na Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, alipofika ofisini kwake Vuga, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi aishukuru EU misaada maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi ameushukuru Umoja wa Ulaya (EU) kwa kuifanya Zanzibar kuwa miongoni mwa maeneo yatakayopata misaada kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maendeleo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar alipozungumza na Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, Jestas Aboud Nyamanga, aliyefika Ikulu Zanzibar kwa kujitambulisha.

Alisema ni jambo jema kwa Zanzibar, husuan kisiwa cha Pemba kuwa miongoni mwa maeneo ambayo miradi ya maendeleo itatekelezwa chini ya ufadhili wa EU, ikiwamo mradi wa 'kuboresha mtazamo wa majiji' (green City), ambao unakusudiwa kutekelezwa katika miji ya Tanga, Mwanza na Pemba.

Rais alisema tangu kuingia madarakani, kumekuwapo dalili za EU kurejesha uhusiano wake na Zanzibar kutokana na kuwapo kwa demokrasia na serikali ya umoja wa kitaifa.

Pia Dk. Mwinyi alisema utalii ni sekta kuu ya uchumi wa Zanzibar, na imejipanga kuimarisha sekta hiyo baada ya kuathirika kutokana na Ugonjwa wa UVIKO-19.

Alimtaka balozi huyo kuendeleza mazungumzo na mamlaka zinazosimamia utalii nchini Ubelgiji ili kufanikisha lengo la kuwapo safari za ndege za kutoka Ubelgiji hadi Zanzibar, hivyo kuleta matumaini ya kuongeza ujio wa watalii nchini.

Akigusia suala la kuwepo fursa za biashara nchini Ubelgiji, Dk. Mwinyi alisema diplomasia ya uchumi inazingatia umuhimu wa kuangalia masuala ya biashara, hivyo akasema pamoja na kuwapo changamoto katika utayarishaji wa dagaa kwa wajasiriamali, serikali itaishughulikia changamoto hiyo hatimaye fursa hiyo kutumika ipasavyo.

Zanzibar, alisema imekuwa ikishughulikia miradi mbalimbali kwa ajili ya maendeleo, hivyo kuwapo kwa taasisi zinazotoa mikopo nafuu ni jambo jema na kubainisha namna serikali itakavyozingatia kupata mikopo hiyo kupitia mashirika hayo ya fedha yaliyoko ndani ya EU.

Naye Balozi Nyamanga alisema kuanza kwa safari za moja kwa moja za ndege kati ya Ubelgiji na Zanzibar kuanzia Oktoba, mwaka huu, kutaongeza idadi ya watalii.

Alisema mawasiliano yamefanyika kuona kunakuwapo usafiri wa ndege ya moja kwa moja kati ya Ubelgiji na Zanzibar kwa wastani wa mara mbili kwa wiki na hivyo kuongeza idadi ya ujio wa watalii baada ya kuathirika kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19.

Kwa mujibu wa balozi huyo, nchi hiyo ina fursa mbalimbali za masomo ya elimu ya juu na kutoa wito kwa vyuo vikuu vya Zanzibar kikiwamo Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kuhamasika ili kutumia fursa zilizopo.

# Walalamikia kukosa kupewa elimu sensa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI zikiwa zimebaki siku 12 kuanza kwa sensa ya watu na makazi, Katibu wa Chama cha Viziwi Zanzibar (CHAVIZA), Abdallah Alawi, amesema bado kundi hilo husussan walioko vijijini linahitaji elimu ya umuhimu wa sensa ili kutoa taarifa sahihi kwa makarani.

Akizungumza na Nipashe mjini Zanzibar jana, Alawi alisema licha ya kwamba serikali kupitia ofisi ya mtakwimu mkuu wa serikali imetoa elimu ya sensa, elimu hiyo zaidi imewafikia viongozi wa taasisi na si viziwi walioko vijijini.

Alisema viziwi wana changamoto kubwa katika kupata taarifa mbalimbali kutokana na changamoto waliyo nayo si rafiki kwa vyombo vya habari.

"Viziwi sisi hatuwezi kusikia mawasiliano kutoka chombo cha habari mfano radio na hata televisheni. Hakuna wakalimani na hata anapowekwa mkalimani mazingira huwa sio rafiki kwao kwa sababu mkalimani huoneshwa katika picha ndogo jambo ambalo ni vigumu kwa viziwi kufahamu kwa haraka kinachozungumzwa" alisema Alawi.

Alisema chama chao kimeshindwa kuwafikia viziwi walioko vijijini kuwapa elimu ya sensa kwa sababu ya nyenzo duni za kufika huko na badala yake elimu hiyo imewafikia walioko mijini pekee.

Pia alisema viziwi wengi waliomba kazi ya ukarani wa sensa lakini waliopata ni wachache licha ya kwamba Zanzibar ina watu wenye ulemavu wa aina hiyo wapatao 2,000.

Aliiomba jamii hasa wazazi kutowaficha watu wenye ulemavu katika kutoa taarifa zao katika wakati wa sensa ili taarifa zao zijulikane na serikali kupanga mikakati imara.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (SHIJIWAZA), Mwandawa Khamis Muhammed, alisema jumuiya hiyo kwa kushirikiana na ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, imetoa elimu ya sensa kwa viongozi wa makundi yote ya watu wenye ulemavu.

Alikiri kuwapo changamoto ya utoaji wa taarifa kupitia vyombo vya habari hasa kwa watu wenye ulemavu wa uziwi jambo ambalo wameshalisema sana hasa kuhusu wakalimani katika vyombo vya habari ambalo ni jambo muhimu ili nao kupata taarifa sahihi.

Naye Ofisa Uhusiano wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salama Njani, alisema ofisi hiyo imewashirikisha kikamilifu watu wenye ulemavu kwa kuwapatia elimu ya sensa kwa makundi mbalimbalii ya watu wenye ulemavu wakiwemo viziwi.


Alisema elimu hiyo waliitoa kwa viongozi wa makundi hayo ili na wao kuishusha katika jamii kwa sababu haiwezi kuwafikia watu wote kwa wakati mmoja ndiyo maana imeyatumia makundi mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari ambao ndio wanafikisha ujumbe kwa haraka.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOSHUA PHILIMON MAZUNGURU** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER NYEUSI** yenye namba za usajili **MC484CUE, CHASIS NO. MD2B15BXOLWJ87829, ENGINE NO. JVXWLJ15646** Yeyote atakayeiona apige simu **0684092643** au atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi kupitia **CONTROL NO: 9910833854356**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVA SIYAMBI MWAMAHONJE a**natangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1420/0043** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KAYUKI SECONDARI SCHOOL** mwaka **2019** .kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DOD/DOD/RB/256659/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**AGATHA JULIUS CHAMI** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma vya; kidato cha nne chenye **INDEX NAMBA: S.2315-0002** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KANDOTO SAYANSI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0248-0544** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MARIAN GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka **2015**

**POLISI TAARIFA: 9910833643699**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na......47/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MONICA KARIST ANDEREA WA KOLA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**YALIYOLETWA NA JIMMY JOHN MSIMBE**

**TANGAZO**

(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 12 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 11 mwezi 08 mwaka 2022**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**HAKIMU MFAWIDHI**

## MNADA WA HADHARA MARUDIO

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD,** Dalali tajwa hapo chini tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana za mdaiwa Sugu Ismail Abdallah Magari kama ilivyotangazwa kwenye gazeti;-

| Mdaiwa/ mdhamini | Dalali | Aina ya Dhamana | Tarehe ya mnada - Mahali |
|---|---|---|---|
| Ismail Abdallah Magari | MMAuctioneers And Debt Collections And Co.Ltd | Toyota Coaster T.915 BXN | 19/08/2022 Mwanza Yard |

**Masharti ya Mnada**

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**0718 730242 / 0677001063**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA CHAMWINO, MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA NDOA Na.22...2022**
**JINA LA MDAI: MWAMINI R. CHILONGOLA**
**JINA LA MDAIWA: BATHOLOMEO UHENGE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa:BATHOLOMEO UHENGE.

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Madai ya kwamba anadai talaka.Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 16/08/2022 saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10/08/2022**

HAKIMU

## KUPOTEA KWA CHETI



**YAHAYA AHMEDI,** Anatangaza kupotelewa na cheti chake cha Kidato cha Nne chenye index no **S.0549-0177** kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia Shule ya Sekondary Lugoba Mwaka 2009. Yeyote atakaekiona ataoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/247502/2022**

**IN THE HIGH COURT IF TANZANIA**
**LAND DIVISION**

**MISC LAND/APPEAL/APPLICATION**
**CASE NO 8 OF 2022**
**RAMADHANI KASONSO**
**PLAINTIFF/APPELLANT/APPLICATION**
**VERSUS**
**ALBINA C/O FRANCIS.......**
**DEPENDANT/RESPONDENT**
**TO ALBINA % FRANCIS**
**P O.BOX**
**MPANDA**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed hearing on the 5 day of 10 2022 at 09:00 am before Hon **JF NKWABI judge.**

**YOU ARE** required to appear in this Court on the fixed date without fail.

Given under my hand and the seal of the court this **5 day of 8. 2022.**

**DEPUTY REGISTRAR**
**HIGH COURT OF TANZANIA SUMBAWANGA**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Taiwan yaanza mazoezi kijeshi baada ya China kusitisha luteka

**TAIPEI,** TAIWAN

Jeshi la Taiwan limefanya mazoezi ya ufyatuaji wa makombora baada ya China kusitisha luteka zake za kijeshi katika kisiwa hicho.

Mazoezi hayo ni kama kujibu kitisho cha kukirudisha kisiwa hicho chenye utawala wa kidemokrasia chini ya udhibiti wake.

Msemaji wa jeshi la Taiwan Lou Woei-jye, aliliambia shirika la habari la Ufaransa AFP kuwa, jeshi la nchi hiyo limefanya mazoezi hayo kama sehemu ya matayarisho ya kujilinda.

Luteka hizo zilizofanyika katika kaunti ya kusini mwa Taiwan ya Pingtung zimeanza mwendo wa saa mbili na nusu na kudumu kwa takriban saa moja.

China ilighadhabishwa na ziara ya spika wa bunge la Marekani Nancy Pelosi, katika kisiwa hicho iliyofanyika wiki iliyopita na kama jibu.

Mzoezi hayo makubwa ya kijeshi ilisababisha kuibuka kwa mvutano wa kiwango cha juu kuwahi kushuhudiwa. Taiwan kwa upande wake imetuhumu China kwa kutumia ziara hiyo kama kisingizio cha kuanza luteka za kijeshi kwa ajili ya kufanya uvamizi. **DW**

## Marekani, Rwanda kuzungumzia waasi 23

**KIGALI,** RWANDA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken amewasili nchini Rwanda katika juhudi za nchi yake ya kuutatua mzozo kuhusu madai ya nchi hiyo kuwaunga mkono waasi wa M23.

Waasi hao wanaoendesha harakati za kivita katika nchi jirani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kusababisha mauaji na watu kukimbia makazi yao..

Blinken pia anatarajiwa kuishinikiza Rwanda kumwachilia Paul Rusesabagina, mhusika wa filamu ya Hotel Rwanda iliyoteuliwa katika tuzo za Oscar Hotel Rwanda.

Hata hivyo, serikali ya Marekani ilisema amezuiliwa kimakosa nchini Rwanda.

Rusesabagina alihukumiwa kifungo cha miaka 25 jela kwa ugaidi na mahakama ya Rwanda mwaka jana katika kile ambacho wafuasi wake walikiita kesi ya uongo.

Wizara hiyo ilisema, Blinken atakutana na viongozi wa Rwanda na wanachama wa mashirika ya kiraia kuhusu masuala mbalimbali muhimu.

Akijibu kwenye ukurasa wa Twitter kuhusu shinikizo linalotarajiwa na Marekani, Rais Kagame alisema, "Hakuna wasiwasi...kuna mambo ambayo hayafanyiki hivyo hapa!!"

Blinken aliwasili Kigali Jumatano usiku kutoka Kinshasa ambapo mamlaka iliiomba Marekani kuiwekea vikwazo Rwanda kwa kuwaunga mkono waasi wa M23 ambao sasa wanadhibiti sehemu za jimbo la Kivu Kaskazini mashariki mwa DR Congo.

Rwanda imekana kuunga mkono kundi la M23, na waasi hao wanakanusha madai kwamba walipigana pamoja na wanajeshi wa nchi hiyo. **BBC**

# Russia yadaiwa kuwalenga raia

**KYIV,** UKRAINE

MAOFISA wa serikali ya Ukraine, wamesema makombora ya Russia yanawalenga raia na wanajeshi kwa pamoja katika mkakati wake wa kudhibiti kamili eneo la Luhansk na Donetsk.

Inaarifiwa kwamba maroketi 120 ya-merushwa katika mji wa Nikopol usiku wa kuamkia jana pekee.

Gavana wa eneo la Dnipropetrovsk, Valentyn Reznychenko alisema watu watatu wameuwawa na wengine saba kujeruhiwa baada ya shambulizi la maroketi katika eneo hilo .

Jana kumeripotiwa mapigano makali katika mji wa mashariki wa Pisky na eneo la magharibi.

Ukraine imeituhumu Russia kwa kuficha silaha zake katika kiwanda cha nyuklia ili kuzilinda.

Ofisa wa Jamhuri ya Watu wa Donetsk, inayoungwa mkono na Russia alisema, eneo la Pisky liko chini ya udhibiti wa majeshi ya Russia na Waukraine wanaotaka kujitenga.

Wakati mapigano hayo yakiendelea, Rais Vladimir Putin, anaendelea kuweka nguvu na uungwaji mkono na nchi za Afrika, na jana alizungumza kwa simu na kiongozi wa mpito wa Mali Kanali Assimi Goïta.

Katika chapisho kwenye Twitter, Goïta alisema "Tulizungumza kuhusu Shirikisho la Urusi kuunga mkono serikali ya mpito kisiasa, na nilisifu ubora wa ushirikiano wetu, ambao unaheshimu uhuru wa Mali na matarajio ya watu wake."

Jumanne, jeshi la wanahewa la Mali lilizindua rasmi ndege kadhaa mpya za kivita zilizotolewa na Russia wakati wa hafla iliyoongozwa na Rais Goita katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Bamako.

Ndege za kivita za enzi ya Usovieti ni kundi la hivi karibuni za usafirishaji wa kijeshi kutoka nchini humo chini ya uhusiano wa karibu kati yake na Mali tangu jimbo la Sahel lilipokumbwa na mapinduzi Agosti 2020.

Mali imeegemea Russia baada ya kutofautiana na nchi za Magharibi, hususan Ufaransa, ambayo inapinga uwepo wa mamluki wa Wagner katika ukanda wa Sahel. **DW**



Vikosi vya usalama nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, vinawasaka zaidi ya wafungwa 800 waliofungwa katika gereza kuu la Kakwangura katika jimbo la Kivu Kaskazini baada ya kutoroshwa na waasi wenye silaha. **PICHA: BBC**

# Mbunge ashinda akiwa mafichoni

**NAIROBI,** KENYA

MBUNGE wa Kimilili Didmus Wekesa Barasa, ametetea kiti chake kwa tiketi ya chama cha United Democratic Alliance.

Barasa, ambaye ametoroka kwa tuhuma za kumuua kwa kumpiga risasi msaidizi wa mpinzani wake Brian Khaemba wa chama cha DAP-K, wakati wa upigaji kura, alipata kura 26,000 dhidi ya kura 9000 za Khaemba.

Kiti cha ubunge cha Kimilili pia kilikuwa kinawaniwa na Peter Makokha kutoka ODM na Erastus Muchimudi wa Jubilee.

Wagombea wote wanne walioshiriki katika uchaguzi huo, hawakujitokeza wakati wa zoezi la kujumlisha kura.

Mvutano ulikuwa mkubwa katika kituo cha kuhesabia kura za maeneo bunge katika Shule ya Upili ya Wavulana ya St Luke Kimilili, huku kukiwa na mzingiro wa polisi.

Polisi walikuwa tayari kumkamata



mbunge huyo ikiwa angefika katika kituo cha kujumlisha kura.

Baadhi ya wakazi wamemtetea mbunge huyo dhidi ya madai hayo, wakisema kiongozi huyo alikuwa anajilinda.

"Barasa alikuwa analinda, hii si mara ya kwanza kwa watu kujaribu kumuua," alisema Wasilwa Wafula.

Hapo awali, maofisa wa polisi walikuwa wamemkamata ofisa msimamizi wa kituo cha kupigia kura cha Lwanda katika wadi ya Kimilili kwa madai ya kuvuruga kura za urais.

Hata hivyo, aliachiliwa baada ya maafisa wa IEBC na polisi kugundua kuwa kituo hicho kilikuwa na maeneo mawili ya kupigia kura.

Mwendesha mashtaka wa umma amewaambia polisi wamkamate mbunge huyo na kurekodi taarifa

Kulingana na mwendesha mashtaka, Noordin Haji, mbunge huyo bado hajakamatwa na simu yake imezimwa.

Lakini, jana Barasa aliibuka kupitia ukurasa wake wa Twitter kwa kuandika ujumbe unaowashukuru wapiga kura wake kwa kumchagua tena.

**BBC**

# WAPINZANI WA SIMBA QUEENS WATUA, WAHOFIA WENYEJI WAO

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Garde Republicaine (GR FC) kutoka Djibouti kimewasili nchini salama, lakini kimesema kinawahofia wenyeji wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika (Ukanda wa CECAFA), Simba Queens ambayo yanatarajiwa kufanyika hapa nchini kuanzia keshokutwa.

Simba Queens itafungua utepe wa mashindano hayo kwa kuwakaribisha GR FC katika mechi itakayochezwa kuanzia saa 7:00 mchana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa GR FC, Mohammed Abdo, alisema timu yake bado changa na haina uzoefu wa kushiriki mashindano ya kimataifa kama ilivyo kwa wachezaji wa Simba Queens.

**Abdo alisema amejiandaa kupambana katika mashindano hayo na wanatarajia watapata matokeo ya kuridhisha katika kila mechi watakayocheza.**

Kocha huyo alisema anaifahamu Simba Queens, hivyo mazoezi yake yamelenga kuhakikisha wanawazuia washambuliaji wao kupata nafasi ya kufunga mabao kirahisi. "Simba Queens ni timu kubwa ukilinganisha na timu yetu, wachezaji wake wamecheza mechi nyingi za kimataifa, sisi ndio tunaanza kuijenga timu, ninaamini tunaweza kuwafunga au kupunguza idadi ya mabao ya kutufunga," alisema Abdo.

Kuhusu hali ya hewa, Abdo alisema amefurahishwa na hali ya hewa ya sasa ya Dar es Salaam na kuongeza kucheza mchana kwake haitakuwa tatizo.

"Kwetu Djibouti hali ya hewa ni nyuzijoto 45, hii hali ya hewa ya Dar es Salaam si tatizo, kwetu ni nzuri, kwa Djibouti kucheza saa 7:00 mchana isingewezekana, naamini wachezaji wangu wataonyesha uwezo mzuri," alisema kocha huyo.

Aliongeza katika kikosi chake ana wachezaji tisa watatu wanaocheza Timu ya Taifa ya wanawake ya Djibouti na anaamini watasaidia kupata matokeo mazuri.

"Mimi nilikuwa kocha wa timu ya taifa kwa tangu 2014, klabu hii imenichukua ili kuijenga upya, lakini bado ninafanya programu za soka la vijana nikishirikiana na FA ya nchi yetu, tunawajenga wachezaji wanawake," Abdo aliongeza.




Wasanii na wadau mbalimbali walioshiriki katika uzinduzi rasmi wa mchezo wa kubashiri Kitonga Jackpot unaosimamiwa na Kampuni ya Kubashiri matokeo ya mechi za ligi tofauti duniani ya Betika uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Twende Kibingwa yatambulishwa*

**Na Saada Akida**

ILI kupunguza makali ya maisha, Kampuni ya Michezo ya Kubashiri matokeo ya Betika imepanua wigo kwa Watanzania kuvuna fedha katika mechi za ligi kubwa za soka duniani kwenye Kitonga Jackpoti ambayo inatoa fursa mbalimbali ya kujishindia mamilioni. Meneja Mauzo wa Betika, Zawadi Gabriel, alisema Kitonga Jackpoti inashirikisha mechi za EPL, Laliga, UEFA, Seria A na Ligi Kuu Tanzania sanjari na michezo mingine ikiwamo ya Cassino.

"Kwa kuanzia washindi watavuna hadi Sh. milioni 251, na itakuwa ikiongezeka kila wiki," alisema Zawadi jana katika uzinduzi wa Jackpoti hiyo iliyokuwa na kauli mbiu ya Twende Kibingwa uliofanyika jijini.

Alisema katika Kitonga Jackpoti ni rahisi kubadili maisha kwa kuwa milionea au bilionea kwa Sh. 2,000 ambayo inatoa fursa ya kuvuna hadi Sh. milioni 251.

"Si wakati wa kukaa kinyonge, Twende Kibingwa, Kitonga Jackpoti inakupa fursa ya kubadili maisha na kukupa nafasi ya kuwa milionea, hii si ya kukosa," alisema Meneja wa Bidhaa wa Betika, Samwel Lawrence.

Aliyewahi kuwa Msemaji wa Yanga, Anthonio Nugaz, alisema Jackpoti hiyo haijawahi kutokea nchini.

## Mbeya City FC kuanza kibabe

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbeya City FC ya jijini Mbeya unatarajia kutangaza jina la Kocha Mkuu wake mpya ambaye atakiongoza kikosi cha timu hiyo katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/2023.

Kocha huyo mpya atarithi mikoba iliyoachwa wazi na Mganda, Mathias Lule, ambaye sasa ni Kocha Msaidizi wa Singida Big Stars ya mkoani Singida.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Mbeya City, Emmanuel Kimbe, alisema walipokea maombi kutoka kwa makocha mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania na sasa wamefanya uamuzi wa kuteua mkuu huyo wa benchi la ufundi.

Kimbe alisema mchakato huo ulifanywa na kamati maalum iliyoteuliwa na tayari wameshapata jina la kocha mpya ambaye anatoka nje ya nchi huku akiongeza maandalizi ya msimu mpya yalisimamiwa na makocha wasaidizi wa timu hiyo ambao wanaifahamu vyema falsafa ya Mbeya City.

"Tuliunda kamati maalum kwa ajili ya kusimamia mchakato huo, walipitia maombi na taarifa zaidi ya 100 ambazo ziliombwa na makocha kwa ajili ya kutaka kufundisha Mbeya City, tayari ameshapatika mmoja na kesho (leo) tutamtangaza rasmi," alisema Kimbe.

## Raga Tanzania yajipanga kutafuta vipaji

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Chama cha Mchezo wa Raga (Rugby) Tanzania, Jacob Jonas, amesema chama hicho kimejipanga kuutangaza mchezo huo ili ufahamike kuanzia ngazi za chini ili kusaka vipaji vipya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Jonas alisema watahimiza wanachama wao kuuendeleza mchezo huo katika shule mbalimbali za msingi ili ufahamike kirahisi.

Jonas alisema kwa kufanya hivyo itasaidia kutengeneza ajira kwa vijana lakini pia anaamini itawasaidia kupata kikosi kizuri cha Timu ya Taifa.

"Huu mchezo unatakiwa kuanzia shuleni kama ilivyo kwa michezo mingine, tunawataka wenyeviti kufanyia hoja hii kwa sababu inalenga kusaidia kupata wachezaji wazuri watakaounda timu yetu ya taifa," alisema kiongozi huyo.

Alisema watahakikisha wanaongeza umakini katika kuziimarisha klabu zao kwa kuunda timu za vijana za kuanzia umri chini ya miaka 14 hadi miaka 20.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### DE JONG NA CHELSEA

CHELSEA wako tayari kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25 na mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (33), ikiwa Barcelona itaamua kuwauza. (***Sky Sports***)

#### FOFANA ATAJWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inaendelea kufuatilia mpango wa kumsaka mlinzi wa Leicester City, Mfaransa Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 21. (***Times***)

#### UNITED MWANZO MWISHO

KLABU ya Manchester United haijakata tamaa ya kumsajili Frenkie De Jong na wana imani atahamia Old Trafford mara tu watakaposuluhisha suala la malimbikizo ya mishahara ya wachezaji na Barcelona. (***90min***)

#### PIQUE KUCHEZA BURE

MLINZI wa Barcelona, Gerard Pique mwenye umri wa miaka 35 amejitolea kucheza bila malipo ili kuisaidia klabu hiyo kufikia sheria za uchezaji wa haki za kifedha za LaLiga na kusajili wachezaji wao wapya. (***AS***)

#### CHRISTENSEN NJIA MOJA

MLINZI wa Denmark, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 26 na kiungo wa kati wa Ivory Coast, Franck Kessie (25), ambao wote walijiunga na Barcelona msimu huu wa joto, wanaweza kuondoka katika klabu hiyo bila malipo ikiwa hawatasajiliwa kwenye Ligi Kuu Hispania, kabla ya mechi ya kwanza ya LaLiga Jumamosi. (***ESPN***)

#### DEPAY ANUKIA JUVENTUS

KLABU ya Juventus inakaribia kufikia makubaliano na Barcelona kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28. (***Sport***)

#### CITY YAHITAJI MLINZI

KLABU ya Manchester City bado ina nia ya kusajili beki mwingine wa kushoto kabla ya dirisha la usajili kufungwa, bila kujali kama beki wa Anderlecht, Sergio Gomez mwenye umri wa miaka 21 atajiunga na klabu hiyo. (***Manchester Evening News***)

#### KALIMUENDI AKARIBIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inakaribia kufikia makubaliano ya thamani ya euro milioni 25 na Rennes kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Arnaud Kalimuendo mwenye umri wa miaka 20, ambaye analengwa na Leeds United. (***L'Equipe***)

#### UNITED YAKWAMA KWA RABIOT

MPANGO wa Manchester United wa kumnunua kiungo wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Adrien Rabiot kwa pauni milioni 15 umekwama kutokana na matakwa ya mshahara ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. (***Gazzetta dello Sport, via Mirror***)

#### LOKONGA ATAJWA MILAN

AC Milan wameripotiwa kuanza mazungumzo na Mbelgiji wa Arsenal, Sambi Lokonga mwenye umri wa miaka 22 huku wakiendelea kutafuta kiungo. (***Football Italy***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI AKICHAMBUA KIWANGO CHA BENZEMA

## ●●● Asema ndiye mchezaji bora kwa sasa duniani na anastahili kubeba tuzo ya...

**HELSINKI,** Finland

CARLO Ancelotti amemsifia na kusisitiza nyota wa Real Madrid, Karim Benzema ni mchezaji bora wa soka duniani kwa sasa.

Benzema aliifungia Madrid bao la pili katika ushindi wa magoli 2-0 wa Super Cup dhidi ya Eintracht Frankfurt kwenye Uwanja wa Olimpiki mjini Helsinki nchini Finland, juzi.

**Bao hilo limemfanya Benzema kuwa mfungaji bora wa pili wa wakati wote wa klabu hiyo, baada ya kufikisha mabao 324.**

Hilo lilimsukuma mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye alichukua nafasi ya Marcelo aliyeondoka kama nahodha wa Madrid - mbele ya nguli wa Los Blancos hao Raul, huku Cristiano Ronaldo akiwa nafasi ya kwanza kwa kufunga mabao 450.

Tangu kuanza kwa msimu uliopita, Benzema amefunga mabao 45 katika michuano yote akiwa na Madrid.

Hiyo ni hesabu iliyoboreshwa pekee na fowadi mpya wa Barcelona, Robert Lewandowski (50), linapokuja suala la wachezaji kutoka ligi tano bora za Ulaya.

Huku tuzo za Ballon d'Or za mwaka huu zikifanyika kabla ya Kombe la Dunia, Benzema anaonekana ana uhakika wa kutwaa tuzo hiyo.

Katika kikao na waaandishi wa habari kabla ya mechi Jumanne, Benzema alieleza hawezi kusema yeye ndiye bora zaidi duniani, kwani anawaachia wengine kuamua.

Alipoulizwa katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi kama Benzema ambaye alipiga mashuti manne na kutengeneza nafasi tatu katika ushindi wa Madrid Jumatano - anaweza kuchukuliwa kuwa mchezaji bora zaidi duniani, Ancelotti alijibu bila kusita.

"Nadhani (yeye ndiye bora zaidi), ndio,"

Ancelotti alisema. "Yeye ndiye mchezaji wetu muhimu zaidi kwa sasa, mchezaji bora zaidi duniani kwa sasa.

"Karim alikuwa mchezaji muhimu zaidi katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa hakufunga katika fainali, lakini mabao yake yalitufikisha fainali, dhidi ya Manchester City na Chelsea na dhidi ya Paris Saint-Germain.

"Yeye ni muhimu sana kwetu. Hakuna shaka, kwa sasa, ni mchezaji bora zaidi duniani."

Ancelotti pia alikuwa kocha wa kwanza kushinda Kombe la Super Cup mara nne tofauti.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,021,2

MECHI KALI
SC FREIBURG
VERSUS
BORRUSIA DORTMUND
1 | 2.99
X | 3.54
2 | 2.16

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# CHELSEA YAKARIBIA KUMNASA DE JONG

**LONDON,** England

CHELSEA wanakaribia kufikia makubaliano na Barcelona kuhusu uhamisho wa Frenkie de Jong, lakini bado hawajashawishika anataka kuondoka katika klabu yake kwa sasa, kwa mujibu wa 90min.

Klabu hiyo ya London Magharibi wiki za hivi karibuni imejiunga kwenye mbio za kuwania saini ya nyota huyo pamoja na wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Manchester United.

United tayari wamekubali ada ya euro milioni 85 kumsajili mchezaji huyo, ingawa hawajaendeleza mpango huo zaidi kutokana na suala la malimbikizo ya mishahara ambayo bado inadaiwa na De Jong.

Vyanzo vya habari vimeonyesha United wana imani mchezaji huyo atajiunga nao iwapo suala hilo litatatuliwa, lakini Chelsea sasa wanaonyesha ushindani mkubwa.

De Jong amezungumza na kocha wa United, Erik ten Hag mara kadhaa na klabu hiyo ya Old Trafford bado haijakata tamaa kuhusu mchezaji huyo, hata kama inalenga dili za viungo wengine ambao ni Adrien Rabiot, ambaye atajiunga kutoka Juventus.

Chelsea sasa wanasonga mbele katika harakati zao za kumnunua De Jong na wanakaribia kuweka dili lao wenyewe kwa mchezaji huyo, ingawa hawatawasilisha ofa rasmi hadi itakapoonyeshwa atajiunga nao.

United bado haijakubali kugharamia gharama zote za mishahara ya malimbikizo ya De Jong - ambayo ni euro milioni 17.

Chelsea, kwa upande wake, iko tayari kugharamia gharama zote za malimbikizo ya mishahara ili kufanikisha mpango huo.

# *Lukaku aelezea hasira zake*

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku amefichua kurejea kwake kwa kukatisha tamaa Chelsea kumemwacha na hasira na sasa anatakiwa kuthibitisha thamani yake ndani ya Inter Milan.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alirejea San Siro mapema msimu huu wa joto baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 97.5 kwenda Chelsea kutokuwa wa mafanikio ambapo alifunga mabao nane tu katika mechi 26 za Ligi Kuu England.

Lukaku hakuwa chaguo la kwanza na kocha wa Chelsea, Thomas



Tuchel akipendelea zaidi kumwanzisha, Kai Havertz, na ikawa dhahiri Mbelgiji huyo hangeweza kulazimisha kurudi kwenye mipango ya kocha huyo wa Ujerumani.

Sasa amerejea Inter k
mkopo wa msimu mzima
Lukaku amekiri kushind
kwake Stamford Bridge ku
washa moto ndani yake.

"Msimu wa Chelsea ulim
motisha zaidi ya kufanya
zuri zaidi kuliko hapo aw
alisema.

"Nadhani katika mw
mmoja kila mtu amesa
kuhusu vitu ambavyo n
uwezo wa kufanya uwanja
"Hiyo ni aina ya hasira
bayo ninayo ndani yar
Kwamba sasa timu ina ma
mengi sana."

HABARI MICHEZO

208,577/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/08/2022 | 17:00 | Brighton vs Newcastle | 2.40 | 3.24 | 2.94 |
| 02. 13/08/2022 | 17:00 | Southampton vs Leeds | 2.24 | 3.39 | 3.09 |
| 03. 13/08/2022 | 17:00 | Wolverhampton vs Fulham | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 04. 13/08/2022 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.37 | 3.19 | 3.04 |
| 05. 13/08/2022 | 17:00 | Sunderland vs QPR | 2.31 | 3.38 | 2.98 |
| 06. 13/08/2022 | 17:00 | Blackpool vs Swansea | 2.36 | 3.28 | 2.98 |
| 07. 13/08/2022 | 21:45 | AC Monza Brianz vs Torino | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 08. 14/08/2022 | 13:15 | FC Volendam vs NEC Nijmegen | 2.53 | 3.47 | 2.63 |
| 09. 14/08/2022 | 15:00 | Viborg FF vs Silkeborg IF | 2.83 | 3.48 | 2.36 |
| 10. 14/08/2022 | 16:00 | Middlesbrough vs Sheffield Utd | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 11. 14/08/2022 | 16:00 | Troyes vs Toulouse | 2.58 | 3.17 | 2.73 |
| 12. 14/08/2022 | 16:00 | AJ Auxerre vs Angers | 2.28 | 3.11 | 3.21 |
| 13. 14/08/2022 | 16:30 | Mainz vs Union Berlin | 2.29 | 3.26 | 3.06 |
| 14. 14/08/2022 | 17:00 | Blackburn vs West Bromwich | 2.41 | 3.29 | 2.89 |
| 15. 14/08/2022 | 18:05 | Nice vs Strasbourg | 2.23 | 3.21 | 3.21 |
| 16. 14/08/2022 | 18:30 | Chelsea vs Tottenham | 2.22 | 3.33 | 3.18 |
| 17. 14/08/2022 | 18:30 | Cadiz CF vs Real Sociedad | 3.13 | 3.13 | 2.35 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 12 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 1162 | Melbourne Knights vs Altona Magic SC | 2.24 | 3.39 | 2.80 |
| 13:00 | 1565 | Kingborough Lions vs Hobart Zebras | 1.23 | 6.25 | 7.82 |
| 13:00 | 5110 | Changwon City vs Cheonan City FC | 2.09 | 2.86 | 3.69 |
| 13:00 | 5668 | Mokpo City vs Siheung Citizen FC | 3.24 | 3.00 | 2.18 |
| 14:00 | 1785 | CLB BD Thanh Hoa vs Hong Linh HA Tinh FC | 1.86 | 3.30 | 3.84 |
| 14:30 | 3281 | Wuhan Three Towns FC vs Beijing Guoan | 1.27 | 5.08 | 8.60 |
| 14:45 | 4761 | Balestier Khalsa vs Hougang United | 2.85 | 4.30 | 2.01 |
| 15:00 | 1559 | Shijiazhuang vs Shandong Luneng | 7.64 | 4.70 | 1.32 |
| 15:00 | 2543 | Guangzhou Evergrande vs Chengdu Qianbao | 8.26 | 4.43 | 1.33 |
| 15:00 | 5366 | Bangkok Utd vs Khon Kaen United FC | 1.24 | 5.47 | 8.99 |
| 18:00 | 4989 | Bkma Yerevan vs Artsakh | 3.58 | 3.28 | 1.94 |
| 18:30 | 5050 | Aluminium Arak vs Havadar | 2.35 | 2.60 | 3.70 |
| 19:00 | 2112 | FK Atmosphere vs FA Siauliai B | 2.21 | 3.69 | 2.65 |
| 19:00 | 2745 | Miedz Legnica vs Zaglebie Lubin | 2.71 | 3.10 | 2.45 |
| 19:00 | 4138 | Radnicki Nis vs Novi Pazar | 1.94 | 3.50 | 3.60 |
| 19:00 | 4897 | FM Auska Alytaus vs FK Ekranas | 1.63 | 3.87 | 4.41 |
| 19:10 | 1273 | Admira Wacker vs Austria Vienna II | 1.46 | 4.33 | 5.51 |
| 19:10 | 5084 | SKN St Polten vs Sturm Graz II | 1.57 | 3.89 | 4.82 |
| 19:30 | 1838 | Fremad Amager vs Naestved BK | 2.50 | 3.33 | 2.50 |
| 19:30 | 2225 | Fakel vs Ural Yekaterinburg | 2.01 | 3.36 | 3.51 |
| 19:30 | 2987 | Hobro vs Sonderjyske | 4.14 | 3.64 | 1.71 |
| 19:30 | 4644 | FC Fredericia vs Vejle BK | 3.29 | 3.58 | 1.93 |
| 19:30 | 4719 | Kaiserslautern vs Paderborn | 2.66 | 3.41 | 2.44 |
| 20:00 | 3096 | Sandefjord vs Rosenborg | 4.32 | 3.97 | 1.69 |
| 20:00 | 3675 | Horsens vs Midtjylland | 4.42 | 3.66 | 1.74 |
| 20:30 | 2089 | Maritzburg Utd vs Moroka Swallows FC | 2.49 | 2.85 | 3.05 |
| 21:00 | 1035 | De Graafschap vs VVV Venlo | 1.49 | 4.39 | 5.39 |
| 21:00 | 1301 | Trabzonspor vs Hatayspor | 1.54 | 4.11 | 5.42 |
| 21:00 | 1607 | HNK Sibenik vs Istra | 2.17 | 3.28 | 2.99 |
| 21:00 | 1620 | Roda Kerkrade vs Jong Ajax | 1.65 | 4.18 | 4.18 |
| 21:00 | 1707 | Helmond Sport vs Jong AZ Alkmaar | 2.40 | 3.44 | 2.64 |
| 21:00 | 2168 | Almere City vs FC Oss | 1.44 | 4.60 | 5.80 |
| 21:00 | 3951 | FC Eindhoven vs Willem II Tilburg | 2.59 | 3.28 | 2.54 |
| 21:00 | 4430 | Telstar vs PEC Zwolle | 3.69 | 3.64 | 1.85 |
| 21:00 | 5209 | Debreceni VSC vs Vasas SC | 2.38 | 3.23 | 2.70 |
| 21:00 | 5850 | SBV Excelsior vs Vitesse Arnhem | 3.30 | 3.60 | 2.00 |
| 21:30 | 3274 | Widzew Lodz vs Legia Warszawa | 3.78 | 3.38 | 1.85 |
| 21:30 | 3901 | SC Freiburg vs Borussia Dortmund | 2.99 | 3.54 | 2.16 |
| 21:45 | 1571 | Derry City vs Shamrock Rovers | 2.74 | 3.08 | 2.44 |
| 21:45 | 3497 | Cork City vs Treaty United | 1.31 | 4.83 | 7.69 |
| 21:45 | 3590 | Oostende vs KAA Gent | 4.32 | 3.72 | 1.74 |
| 21:45 | 3937 | Bohemians FC vs Dundalk FC | 2.49 | 3.13 | 2.64 |
| 21:45 | 4191 | Dundee FC vs Arbroath | 1.85 | 3.33 | 4.08 |
| 21:45 | 5994 | UCD Dublin vs Finn Harps | 3.14 | 3.14 | 2.16 |
| 22:00 | 1741 | Watford vs Burnley | 2.29 | 3.16 | 3.06 |
| 22:00 | 2926 | Osasuna vs Sevilla FC | 3.09 | 3.04 | 2.40 |
| 22:00 | 4797 | Nantes vs Lille | 2.77 | 3.22 | 2.48 |
| 22:00 | 5306 | Copenhagen vs Randers | 1.48 | 4.40 | 5.80 |
| 22:00 | 5863 | Levante vs Huesca | 1.62 | 3.70 | 5.20 |
| 22:15 | 3170 | Famalicao vs Sporting Braga | 3.17 | 3.37 | 2.16 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# POLISI TANZANIA KUIVAA YANGA KWA TAHADHARI

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Polisi Tanzania imeondoka Dar es Salaam na kuelekea mkoani Kilimanjaro kuendelea na maandalizi ya kuwakabili mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Yanga kwa ajili ya kuwakaribisha katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa Agosti 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wamepata mazoezi ya kutosha katika kambi iliyokuwa hapo jijini na sasa wako tayari kuwakabili Yanga.

Mketo alisema mechi mbalimbali za kirafiki walizocheza zimewasaidia kukijenga kikosi chao na wanaamini wataendeleza matokeo mazuri dhidi ya mabingwa hao ambao msimu uliopita hawakupoteza mchezo hata mmoja.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wote wanaendelea vyema huku akifurahishwa na ushindani wa kuwania namba unaoonekana mazoezini wenye lengo la kuondoka na pointi tatu kwenye mechi hiyo ya kwanza ya msimu mpya.

Aliongeza mapungufu madogo madogo ambayo wameyabaini katika michezo ya kirafiki inayoendelea kufanyiwa kazi ili kufikia malengo ya kuanza msimu mpya kwa kuondoka na pointi tatu.

"Makosa madogo madogo ya kiufundi ambayo tumeyaona katika michezo ya kirafiki tunaendelea kuyafanyia kazi mpaka ikifika siku ya mchezo dhidi ya Yanga, kila kitu kitakuwa sawa," alisema kocha huyo.

Alisema anaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kwa sababu anafahamu watakutana na Yanga ambayo imejiimarisha zaidi msimu huu lakini ikijiandaa kuendeleza pale walipoishia.

Polizi Tanzania imepoteza mechi ya kirafiki dhidi ya Namungo FC kwa kukubali kichapo cha mabao 2-0.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (kulia), akiwa na viongozi wengine mbalimbali wakifuatilia hotuba ya Rais wa FIFA, Gianni Infantino, katika Mkutano Mkuu wa 44 wa shirikisho la mchezo huo Afrika (CAF), uliofanyika jijini Arusha juzi. **PICHA: TFF**

# Zahera apigia debe vijana

**Na Adam Fungamwango**

MKURUGENZI wa Ufundi wa Yanga, Mwinyi Zahera, amezitaka klabu zote hapa nchini kutengeneza wachezaji vijana kwa ajili ya kuwaandaa kuwa wanasoka nyota wa baadaye na si kubakia katika vita ya kushinda vikombe pekee.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Zahera, alisema amekuwa akiwatengeneza wachezaji vijana chini ya miaka 17 na miaka 20 kwa ajili ya kuwabadilisha na kuwa wachezaji wenye uwezo na maarifa makubwa.

"Soka la vijana ni kama shule, huko kuna wa kwanza hadi wa mwisho huku walimu wakiangalia namna ya kuwaendeleza wale walio juu na kuwarekebisha waliko chini ili nao viwango vyao vipande.

"Hakuna klabu ambayo inatengeneza wachezaji wa umri chini ya miaka 17 na miaka 20 wote waje kuwa nyota, ndiyo maana unaona timu nyingi kubwa duniani zina wachezaji vijana, lakini si wote wanaokwenda kuchezea timu kubwa au kuwa nyota," alisema Zahera.

Aliongeza naye anawatengeneza wachezaji katika klabu hiyo kwa mfumo huo na anazikumbusha timu nyingine kufuata nyayo hizo badala ya kujipanga kushinda mataji pekee.

"Na hata mazoezi ninayowapa, hatufanyi kwa ajili ya kuchukua ubingwa, ni yale ya kuwajenga watoto na kuwapata hata wawili watatu ambao wanaweza kwenda timu kubwa, hiyo falsafa ya mafunzo kwa wachezaji vijana duniani kote," alisema Mkongomani huyo.

# Michezo

Nipashe Ijumaa Agosti 12, 2022




**Chelsea yakaribia kumnasa de Jong**

UKURASA 22



Rais wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Gianni Infantino (katikati), akimwagilia mti wa matunda aliopanda kuhamasisha utunzaji wa mazingira jijini Arusha jana. Kushoto ni Rais wa Shirikisho la Mchezo huo Afrika (CAF), Dk. Patrice Motsepe na Rais wa TFF, Wallace Karia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Simbu mawazo yahamia Olimpiki

**Na Shufaa Lyimo**

MSHINDI wa medali ya fedha, Alphonce Simbu, amesema amefurahi na kushukuru kupata medali hiyo katika mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika hivi karibuni mjini Barmigham, Uingereza.

Simbu aliliambia gazeti hili kufanya vizuri katika mashindano hayo ni chachu nyingine kwake kuelekea kwenye Michezo ya Olympiki itakayofanyika mwakani jijini Paris, Ufaransa.

"Mafanikio haya yametokana na maandalizi ya muda mrefu tuliyofanya kwa usimamizi wa serikali, tunaomba wadau wengine washirikiane na serikali ili kufanikisha safari hiyo tupate medali za olympiki," alisema Simbu.

Mwanariadha huyo alisema matokeo mazuri yatawapa wanariadha wachanga moyo wa kufanya vizuri zaidi baada ya kuona mafanikio yanayonekana katika mchezo huo.

Naye bondia wa ngumi za ridhaa, Yusuph Changalawe, ambaye alipata medali ya shaba alisema amefurahi kupata medali hiyo licha ya kuwa haikuwa kazi rahisi.

"Mashindano yalikuwa na ushindani sana, nashukuru kwa matokeo haya, ninaahidi Watanzania nitaendelea kufanya vizuri katika mashindano mengine ya kimataifa," Changalawe alisema.

# Simba, Yanga hesabu kali

## Makocha wao waendelea kuumiza vichwa, ulinzi mkali waandaliwa ili...

**Na Waandishi Wetu**

KUELEKEA mechi ya kuwania Ngao ya Jamii itakayowakutanisha watani wa jadi nchini, Yanga na Simba, makocha wa timu hizo wameendelea kutamba vikosi vyao vimeimarika, lakini kila upande ukijiandaa kuzidisha umakini ili kuhakikisha wanatimiza malengo ya kuondoka na ushindi katika mchezo huo.

**Yanga inatarajia kuikaribisha Simba katika mechi hiyo ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2022/2023 itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amewataka wachezaji wake kucheza kwa kujituma zaidi ili kufikia malengo ya kuwafunga wapinzani wao, Simba ambao pia wanaonekana ni wenye ubora.

Nabi alisema kiwango kilichoonyeshwa na Simba katika mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa kwenye Tamasha la Simba Day dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu Ethiopia, St. George lilimpa mwangaza mahali ambapo wapinzani wao walipo.

"Utakuwa mchezo mgumu na wenye changamoto mbalimbali, kila timu ina wachezaji wazuri, wenye uzoefu lakini wenye kiu ya kupata matokeo bora, ili ufikie huko ni lazima tuwe watulivu na tucheze kwa tahadhari wakati wote," alisema Nabi.

Taarifa kutoka katika kambi ya Yanga zinasema Nabi amefanya kikao na wachezaji wake na kuwataka wawe makini katika mchezo huo kwa sababu Simba ni timu ngumu.

"Kocha Nabi amewataka wachezaji wajitume katika mazoezi ili wahakikishe wanaibuka na ushindi Jumamosi, amesema anaijua Simba ni timu nzuri na ngumu kutokana na alivyoiona katika mechi yake dhidi ya St.George, anaiheshimu, anasisitiza zaidi wachezaji utulivu ingawa anakiamini kikosi chake kinaweza kupata ushindi katika mchezo huo," kilisema chanzo chetu.

Kiliongeza mabosi wa timu hiyo wakiongozwa na Rais, Injinia Hersi Said, leo wanatarajia kukutana na wachezaji ili kutoa ahadi yenye lengo la kuwaongezea hamasa kuelekea mchezo huo.

Naye Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kuwakabili wapinzani wao na amekamilisha hesabu za kuelekea mechi hiyo muhimu.

"Tumefanya kila kitu muhimu, tunaamini tutapata matokeo mazuri, wachezaji wangu wanaendelea kunivutia kila siku, ninaamini hawatawaangusha mashabiki wao," alisema Maki.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' amesema wanajivunia kuwa na kikosi imara.

"Dabi ni mchezo usiotabirika, tunawaheshimu Yanga, lakini kwa sasa tuna timu nzuri kuliko wao, mechi tofauti sana, lakini tumejipanga kushinda," Try Again alisema.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema litachukua tahadhari zote za kiusalama kabla, wakati na baada ya mchezo wa Ngao ya Jamii ili kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Kamanda wa Kanda Maalum, Jumanne Muliro, alisema wamejipanga kuhakikisha usalama unakuwa wa kiwango cha juu huku akiongeza hakutakuwa na mtu au kikundi chochote kitakachoruhusiwa kuingia na silaha ya aina yoyote uwanjani.

Alisema Polisi watazingatia maadili, weledi na kuzitunza siri za wananchi huku akitoa wito kwa jamii kuimarisha mifumo ya ulinzi shirikishi ili kuzuia vitendo vya uhalifu.

Kamanda huyo amewaondoa hofu mashabiki wa soka wanaohofia kufika uwanjani kwa kuwaeleza ulinzi utaimarishwa kwa kiwango cha juu.

**Imeandaliwa na Hadija Mngwai, Saada Akida, Salma Twaha (TUDACo) na Jackson JACOB (UDOM).**

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >